SportPesa
TZS. 761,374,640
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#

**Viongozi wa dini wakemea biashara ngono watoto wadogo**




UKURASA 3

**MAISHA** Nipashe Jumapili — Baba, Mama na Mwana



PUNGUZA UZITO
Kwa juisi ya tango



NYUMBA:
Jifunze namna ya kusafisha sofa



HARUSI



KARABATI NGOZI
**Tango, nyanya, asali vinatosha kukupa furaha**

Jumapili Desemba 12, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580792
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Presha yapanda mawaziri

**Baada** ya Rais Mwinyi kuanika ujio mabadiliko, atetea kampuni ya kigeni kuendesha uwanja wa ndege...*Endelea ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



UKURASA 3

Mbunge wa Kuteuliwa na Rais, Humphrey Polepole

## Polepole: Siondoki ng'o CCM, labda wanifukuze wenyewe

## Wadakwa tuhuma mauaji, kunyofoa viungo

UKURASA 3

MICHEZO DTB, IHEFU ZAKARIBIA LIGI KUU UK.23
MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC), Moussa Faki Mahamat, baada ya kuwasili Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Presha juu, chini mawaziri Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

NI presha kupanda na kushuka kwa mawaziri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Ndivyo hali inavyoonekana baada ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kuvunja ukimya kwamba mabadiliko ndani ya baraza hilo ni lazima na hayaepukiki.

Rais Dk. Mwinyi ameweka bayana kuwa wananchi watarajie kufanyika mabadiliko hayo huku akisisitiza kuwa utendaji mzuri wa kazi ndio utakaombakisha waziri kwenye baraza hilo.

Licha ya kugusia mabadiliko kwenye baraza, pia amesema yatawahusu watendaji wengine kwenye taasisi na mashirika ya umma.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu, Zanzibar jana, Rais Mwinyi alisema uzoefu wake wa zaidi ya miaka 20 katika baraza la mawaziri unaonyesha kuwa mabadiliko katika baraza hilo ni jambo la lazima.

"Kwa kipindi chote nilichokaa katika baraza la mawaziri, sijawahi kuona kinaisha kipindi chote cha miaka mitano pasiwapo mabadiliko," alisema.

**KAMPUNI YA KIGENI**

Kuhusu uamuzi wa serikali kuipa kampuni ya kigeni kuendesha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, alisema umelenga kuboresha huduma ambazo zilionekana kuzorota na kusababisha usumbufu kwa watalii.

Alisema uwanja huo ni eneo muhimu kutokana na kuingizia serikali kipato kikubwa kitokanacho na utalii, hivyo huduma zikiwa mbovu zinatishia kushuka kwa mapato hayo kwa kuzingatia ukweli kwamba idadi ya watalii itapungua.

Dk. Mwinyi alisema watalii na wageni mbalimbali wanaotumia uwanja huo walikuwa wakipata usumbufu mkubwa wanapofika uwanjani hapo na wakati mwingine walikuwa wakitumia hadi saa tatu kukamilisha taratibu.

"Kulikuwa na foleni kubwa sana kwa watalii na wageni wetu huduma zilizorota kiasi kwamba mtu anatumia hadi saa tatu kutoka uwanja wa ndege. Sasa tukaona hali hiyo itatupunguzia watalii, hivyo tupate kampuni yenye uwezo itakayosaidia kuondoa matatizo hayo na sina shaka na kampuni hiyo," alisema.

Rais Mwinyi alisema kampuni iliyopewa zabuni hiyo ina uwezo mkubwa kiutendaji na imekuwa ikitoa huduma ya aina hiyo kwenye nchi 26 duniani ikiwamo Uwanja wa Ndege wa Dubai, hivyo serikali haina wasiwasi nayo.

Alisema kampuni hiyo ilipatikana baada ya mchakato wa miezi sita ikishindana na kampuni mbalimbali na itakuwa ikiipatia Serikali ya Zanzibar asilimia 12 ya mapato yatakayopatikana tofauti na asilimia tano ambayo ilikuwa inapata kabla ya ujio wa kampuni hiyo.

**UVIKO- 19**

Kuhusu vipimo vya UVIKO-19 kupewa kampuni binafsi, Rais Mwinyi alisema SMZ ilichukua uamuzi huo baada ya kuona utaratibu wa ovyo wa kuchukua vipimo hivyo kuchukua muda mrefu na kusababisha usumbufu.

Rais Mwinyi alisema awali watu walikuwa wakikaa muda mrefu bila kupata majibu ya vipimo vyao na wakati mwingine baadhi ya watalii walilazimika kuahirisha safari zao kutokana na majibu ya vipimo hivyo kuchelewa.

"Malalamiko yalikuwa mengi sana kwenye vipimo ilifika wakati mtalii anakaa siku nne hajapata majibu ya vipimo vyake na kutokana na kuchelewa vipimo wapo waliokuwa wanalazimika kuahirisha safari zao kwa kusubiri majibu ya vipimo tukaona hii si sawa tumempa mtu binafsi sasa majibu yanapatikana ndani ya saa 24," alisema Rais Mwinyi.

Alisema tangu mtu binafsi apewe zabuni ya kuchukua vipimo hivyo huduma zimeboreshwa, malalamiko yaliyokuwepo yamekwisha na serikali inapata mapato makubwa zaidi ya yale iliyokuwa ikiyapata.

"Kuna wazabuni walitaka wakipata dola 80 watupe dola 10 tu lakini huyu mzabuni wa sasa katika dola 80 anatupa dola 50. Yeye anachukua dola 30 na hizi zinazopatikana nimeagiza zikasaidie kuboresha sekta ya afya na zimeshafanya mambo makubwa sana," alisema

**MADAI VISIWA KUUZWA**

Rais Mwinyi alisema SMZ imeamua kuwapa wawekezaji kujenga hoteli kama njia ya kuvutia watalii na hoteli 600 zilizopo sasa hazitoshelezi mahitaji yaliyopo.

Alisema hakuna sababu ya kuviacha visiwa hivyo vikakaa bila kusaidia uchumi wakati kuna wawekezaji ambao wanaweza kuvichukua na kuwekeza na kusaidia kuvutia idadi kubwa ya watalii ambao watasaidia kukuza uchumi.

"Kwa sasa hatujajitosheleza wageni wanakuja wanakaa vichochoroni tukakaa tukaona kwanini wakati nafasi tunayo na siyo sisi tu wa kwanza kufanya hivi wenzetu kwenye mataifa mbalimbali wamechukua uamuzi kama huu na tumekwenda tumejionea manufaa wanayopata," alisisitiza

Alisema wawekezaji hao hawapewi bure kwa kuwa wamekuwa wakitanguliza fedha nyingi kwa serikali hata kabla ya kujenga hoteli na wengine wametoa hadi dola milioni tatu na kuongeza kuwa wameshafanya hivyo kwa visiwa 10 kati ya 52 vilivyoko Zanzibar.

**MAHAKAMA MAALUMU UKATILI**

Alipoulizwa sababu ya kuongezeka kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji Zanzibar licha ya kuazishwa kwa mahakama maalumu ya kushughulikia vitendo hivyo, alisema huenda kumechangiwa na mwamko wa jamii kutoa taarifa juu ya vitendo hivyo.

Alifafanua kuwa huenda zamani watu walikuwa wanashindwa kujitokeza kuripoti vitendo hivyo kwa sababu walikuwa hawana uhakika kwamba vitashughulikiwa na sasa wanaona kuna chombo maalumu cha kukiamini.

**UCHUMI WA BLUU, MUUNGANO**

Kuhusu uchumi wa bluu, alisema lengo ni kuwapo kwa matumizi endelevu ya bahari ikiwamo kulinda mazingira na wavuvi kunufaika na rasilimali za bahari.

Kwa upande wa Muungano, alisema kuwa hakuna changamoto inayomnyima usingizi katika kero za Muungano kwa sababu kazi kubwa imefanywa katika kuzipatia ufumbuzi kero nyingi.

"Changamoto zinaendelea kuwapo na kutafutiwa ufumbuzi pale zinapojitokeza," alisema.

Alisema baadhi ya kero zilizopatiwa ufumbuzi ni kuwepo kwa mfumo mzuri wa ajira katika taasisi za Muungano na suala la mfuko wa fedha wa pamoja bado linaendelea kufanyiwa kazi kwa sababu linahitaji mda wa pande zote mbili kujiridhisha juu ya mgawanyo wa fedha.

**MAFUTA NA GESI**

Kuhusu sekta ya nishati hususan mafuta na gesi, alisema katika utafiti uliofanyika, imegundulika kuwa Zanzibar ina gesi ya kutosha, hivyo ana matumaini makubwa na rasilimali hiyo.

Alisema uchumi wa Zanzibar utakuwa mkubwa kutokana na rasilimali hiyo na kutakuwa na mtambo wa kusafisha gesi.

Dk. Mwinyi alisema azma yake ya kuingia serikalini ni kuimarisha amani katika nchi, umoja na mshikamano kwa sababu ndio msingi wa maendeleo na kwamba lazima yawapo mazungumzo ya vyama vya siasa ili kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hilo amefanikiwa.

"Nchi yetu ina amani ya kutosha na wananchi wake ni wamoja kwa hiyo hatuna sababu ya kutoleta maendeleo,"alisema.

Alisema ili mambo yaende vizuri na kuleta maendeleo lazima kuwapo uwajibikaji ndiyo maana amefanya mabadiliko mbalimbali ya kiutendaji lengo likiwa kuongeza uwajibikaji ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema ili nchi kupiga hatua ni kuvutia uwekezaji na moja ya vipaumbele vyake ni kuweka maeneo mazuri ya uwekezaji na biashara na kwa sasa nchi ipo katika mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara jambo ambalo limeleta wawekezaji wengi katika sekta mbalimbali.

Pia alisema vipaumbele vyake vingine ni kuimarisha huduma muhimu za jamii na kuondoa kero mbalimbali katika jamii na kusema kero kubwa ni udhalilishaji.

Sambamba na hilo, alisema pia kuna kilio kikubwa cha wananchi kuny'ang'anywa ardhi zao hivyo kumepelekea kuwepo kwa migogoro mingi ya ardhi. Alisema ameunda tume ya kushughulikia kero hiyo na kuitafutia ufumbuzi wa kudumu.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma mauaji kisha kutoa ubongo, ulimi na koromeo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la polisi mkoani Kagera linawashikilia watu wanane kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata mapanga Stella Paschael (51) mkazi wa Nyabihonza wilayani Karagwe, na kisha kutoweka na baadhi ya viungo vyake vikiwamo ubongo, ulimi na koromeo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Awadhi Haji, alisema jana kuwa mauaji hayo yalitokea Desemba 3, mwaka huu, saa 12:00 asubuhi na kwamba baada ya watu hao kutekeleza kitendo hicho, walikimbilia kusikojulikana.

"Baada ya polisi kupata taarifa, uchunguzi juu ya tukio hilo ulianza na kati ya Desemba 6 na 7, watuhumiwa wote wanane walikamatwa, wakahojiwa na kukiri kuhusika na mauaji ya mama huyo," alisema.

Alisema baada ya mahojiano ya kina watu hao, walisema walimuua kwa sababu kuna vifo vya watu wawili vilitokea katika familia zao na walipokwenda kwa mganga wa kienyeji waliambiwa kuwa ndiye anahusika, hivyo kufanya mipango ya kumwua.

Kamanda huyo aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Libert Robert (19), Frank Yese (20), Akiza Ovence (35), Thomas Juma (42), Batalinganya Mathias (30), Jackson Alex (23), Alex Phidel (32) wote wakazi wa Bukangara wilayani Karagwe na John Kwabi ambaye ni mganga wa kienyeji.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani.

"Jeshi la polisi linatoa onyo kwa vitendo hivi vya kihalifu vya mauaji kwa imani za kishirikina. Tunawaomba wananchi kutoa taarifa za watu wanaojihusisha na ramli chonganishi ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria. Tunataka kuepukana na vitendo vya mauaji vinavyochochewa na waganga wa kienyeji," alisema.

# Polepole: Siondoki CCM, nitapambana

**Na Richard Makore,** MWANZA

ALIYEKUWA Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amesema hana mpango wa kuondoka kirahisi katika chama hicho.

Polepole amesisitiza kwamba hana mpango wa kuachia ngazi na kwamba labda wamfukuze wenyewe.

Pia amesema ameajindaa kwa hoja za kisheria kujitetea mbele ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), iliyomwita kumhoji kuhusu vitu anavyozungumza kupitia taasisi yake ijulikanayo kama shule ya uongozi. Taasisi hiyo inarusha maudhui yake kupitia chaneli ya Youtube.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii jana, Polepole alikiri kuitwa na CCM na kuhojiwa na kwamba alijibu hoja zote kwa ufasaha ingawa alisema hawezi kusema alichoulizwa wala alichojibu.

Kwa mujibu wa Polepole, kanuni na taratibu za chama zinazuia mazungumzo hayo kutolewa hadharani kwa kuwa ni ya siri.

"Watu walisema nataka kujiondoa CCM, labda niseme kwamba sikubali kirahisi. Lazima kuwe na mpambano mkali ndani ya chama na kama kutoka wanitolee dirishani," alisema.

Alisema kuna vitu anavisema kwa jamii kwa lengo la kutoa elimu lakini inaonekana haviwafurahishi baadhi ya watu ambao wamefikia hatua ya kumpigia simu na kumtaka aachane na hayo mambo.

Polepole ambaye ni Mbunge wa kuteuliwa, alitaja baadhi ya vitu alivyozungumzia hivi karibuni na kuonekana kama anapingana na serikali kuwa ni pamoja na suala la kuwapanga wafanyabiashara wadogo (machinga) katika maeneo rasmi ya kufanyia biashara. Alisema mambo mengine aliyozungumzia kwa madai ya kutetea maslahi ya nchi ni pamoja na ujenzi wa bandari ya Bagamoyo na kwamba hawezi kunyamaza kusema na kusimamia anachokiamini hata kama ni ubunge wamnyang'anye hana shida nao.

"Mimi niko tayari kuona watu wote wakielekea upande wa kusini na nisiwafuate. Kama kuna vitu sikubaliani navyo, niko tayari kuelekea kaskazini nikiwa peke yangu," alisema. Katika mazungumzo hayo jana, alisema alikwenda Dar es Salaam mwaka 1988 akiwa hana cheo chochote na kwamba suala la madaraka ni jambo la kupita tu kwake.

Hata hivyo, katika mazungumzo yake, Polepole alionekana kutetea mambo mbalimbali yaliyofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya hayati Rais John Magufuli.

Moja ya mambo aliyosema yalifanyika wakati huo ni pamoja na kudumisha mahusiano na mataifa mengine hatua ambayo ilichangia nchi mbalimbali kuendelea kuisaidia Tanzania.

Alitoa mfano wa misaada hiyo kuwa ni pamoja na ujenzi wa bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linatarajiwa kuzalisha megawati zaidi ya 2,000 za umeme, kujenga reli , barabara na sekta nyingine.

Alikanusha kauli za baadhi ya watu wanaosema kwamba katika awamu hiyo uhusiano wa Tanzania na nchi mbalimbali haukuwa mzuri, huku akihoji kama mahusiano yalikuwa mabaya tusingepata misaada hiyo.

Kuhusu uhuru wa watu kusema, alisema katika kipindi cha awamu ya tano uliongezeka kuliko kipindi chochote. Alisema watu walisema kile walichokiamini na walikuwa huru kufanya hivyo, isipokuwa wachache waliosema uongo ndiyo sheria ilipambana nao.

Kuhusu kujitetea mbele ya TCRA, Polepole alisema hawana uwezo wa kumnyamazisha na kwamba alilipia Sh. milioni moja 1 kupata chaneli ya Youtube ambayo inaonyesha maudhui katika taasisi yake ya uongozi.

"Jumatatu (kesho) nitakwenda huko na nondo zangu ili kujitetea na nitasema ukweli na nina hakika hawawezi kunishinda kwa sababu naona nipo sahihi," alisema.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizindua mpango wa 'Women Mean Business Program' katika ukumbi wa Maktaba Mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Geofrey Mwambe, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Mgalula (kulia) na (wa pili kulia) ni Mkuu wa Kitengo cha Ushirikiano,Ubalozi wa Canada nchini, Hellen Fytche. **PICHA: OWM**

# Viongozi wa dini wakemea kushamiri biashara ya ngono kwa watoto wadogo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIONGOZI wa dini kutoka madhehebu mbalimbali Shinyanga, wamelaani kitendo cha watoto wadogo mkoani hapa kufanya biashara ya ngono, huku serikali ikishindwa kuchukua hatua.

Walibainisha hayo juzi wakati wa kongamano la viongozi wa dini na jamii la kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, lililoandaliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria.

Mmoja wa viongozi hao, Sheikh Khalfan Ally, alisema katika mkoa wa Shinyanga biashara ya ngoni kwa watoto wadogo imeshamiri, hasa katika maeneo ya reli, huku wakiwa na mabaunsa wao wakiwalinda.

"Watoto wa kike wanafanyiwa sana ukatili lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Serikali mna 'deal' (mnajihusisha) na watu gani. Mfano pale relini kuna biashara ya ngono dhidi ya watoto wadogo na wanalindwa na mabaunsa. Watu wanafika pale wanatoa Sh. 2,000 wanakwenda kufanya nao ngono," alisema.

Mchungaji Charles Lugembe kutoka Kanisa la Africa Inland Tanzania (AICT) Mjini Shinyanga, alisema ili jamii iondokane na matukio hayo ya ukatili wa kijinsia, ni kuendelea kupaza sauti juu ya vitendo hivyo na kuvikemea kwa nguvu zote.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Dk. Emmanuel Makala, alisema kanisa hilo linachukizwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa mabinti.

Alisema kanisa hilo kwa sasa linatekeleza mpango wa kutokomeza ukatili wa kijinsia, ambao ulianza mwaka 2020 na utakoma mwaka 2024 kwa kutoa elimu ya kujitambua na afya ya uzazi kwa wasichana.

Mbali na utoaji wa elimu hiyo, wamekuwa wakiwawezesha wasichana wakiwamo waathirika wa mimba na ndoa za utotoni na kuwapatia elimu ya ujasiriamali na ushonaji, ili kutimiza ndoto zao na kuendesha maisha hayo.

Alisema wamekuwa wakiwawezesha pia wazazi wanaoishi katika maisha duni, kuwapatia ng'ombe wa maziwa, ili wauze maziwa na kujipatia fedha na kuacha kuwafanyia ukatili mabinti zao ikiwamo kuwaozesha ndoa za utotoni.

Mratibu wa Kudhibiti Ukimwi Mkoa wa Shinyanga, Dk. Peter Mlacha, akizungumza kwenye kongamano hilo, alisema biashara ya ngono ni moja ya sababu ambazo zinachangia mkoa kuwa na kiwango cha juu cha maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) kwa asilimia 5.9 wakati kitaifa ni asilimia 4.9.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo, Beda Chamatata, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, aliwataka viongozi wa dini kuendelea kupaza sauti kupinga ukatili wa kijinsia huku serikali nayo ikiwachukulia hatua watu ambao hutenda ukatili huo.

Alisema takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani hapa kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, mwaka huu yalikuwa 5,845 ambapo watu wazima waliofanyiwa ukatili walikuwa 3,335 na watoto 2,510. Alisema waathirika wakubwa wa matukio hayo ni wanawake na watoto.

## Majaliwa awahimiza makandarasi weledi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka makandarasi na taasisi zingine za sekta binafsi kuzingatia weledi, maadili na uaminifu wakati wa utekelezaji miradi ya maendeleo ili kuleta tija kwenye maisha ya Watanzania.

Amesema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi nchini.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipofungua mkutano wa 21 wa wanachama wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na kongamano la biashara na uwekezaji, katika ukumbi wa maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Sekta binafsi imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, viwanda sanaa, mawasiliano pamoja na utalii," alisema.

Majaliwa alisema serikali itaendelea kuishirikisha sekta binafsi katika ziara za serikali nje ya nchi kama alivyofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye ziara za Kenya, Burundi, Marekani, Malawi, Msumbiji na Uganda.

"Nitumie fursa hii kuwashukuru kwa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia utengenezaji wa ajira, kukuza kipato cha wananchi, kutengeneza bidhaa, kuongeza pato la Taifa na kuongeza uwezo wa nchi kujitegemea.

"Sekta binafsi endeleeni kushiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimkakati, pamoja na kuhakikisha mnawekeza katika maeneo ya vijijini kwa kuanzisha viwanda katika maeneo hayo ili kupunguza idadi ya watu wanaosafiri kuja maeneo ya mjini kutafuta ajira," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema serikali imeendelea kuondoa na kupunguza kodi, ushuru na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji kupitia sheria za fedha kwa vipindi tofauti.

"Katika kuzingatia hayo serikali imepunguza kodi ya sukari ya viwandani kutoka asilimia 15 hadi tano, tozo ya ujuzi kutoka asilimia 4.5 hadi nne, kuwekwa kwa tozo za kulinda viwanda vya Tanzania pamoja na kodi ya forodha ya mafuta ghafi ya chakula ambayo imeongezwa maradufu ili kuimarisha ushindani na kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini," alisema.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amesema licha ya uwekezaji kuendelea kukua nchini Watanzania wameendelea kuwa wadau muhimu kwa kuwa hadi sasa usajili wa zaidi ya asilimia 43 ya wawekezaji ni wazawa.

# Ukosefu lishe bora wadaiwa ni ukatili

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

UKOSEFU wa lishe bora umeelezwa kuwa ukatili kwa watoto kwa kuwa unawasababishia udumavu wa akili na mwili.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Mwajuma Magwiza, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo kuhusu programu jumuishi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa wataalamu wa sekretarieti za mikoa nchini.

Alisema jamii haina budi kuelimishwa namna bora ya malezi kwa watoto katika kila hatua kitaalamu zaidi ili kuwajengea misingi imara ya ukuaji na ujifunzaji.

Magwiza alisema pamoja na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa watoto vinavyoripotiwa bado ni vichache, vitendo hivyo vinasababisha ongezeko la udumavu.

"Kuanzishwa kwa programu hii kunawajumuisha wataalamu wakiwamo madaktari ambao wana sayansi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, hivyo watatusaidia katika kuelimisha jamii.

"Tunajua kila mzazi anaamini anatoa malezi kwa usahihi lakini kuna hatua za malezi za kitaalamu ambazo jamii inapaswa kujengewa na washiriki wote humu kutokana na utaalamu wenu. Huduma za malezi zinatakiwa zimjengee mtoto afya, lishe, ujifunzaji na mwitikio," alisema Magwiza.

Magwiza alisema lengo la programu hiyo ni kujenga uelewa wa pamoja kuifahamu vizuri ili itapozinduliwa utekelezaji uanze kwa pamoja wote wakiwa na uelewa. Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mtoto, Sebastian Kitiku, alisema lengo la programu hiyo ni muhimu katika utekelezaji wake hasa kwa mshiriki wakiwamo maofisa lishe, maafisa elimu, maofisa maendeleo na ustawi wa jamii na waganga wakuu wa mikoa.

Alisema vitabu kuhusu programu vimeandaliwa kwa lugha zote mbili lengo ni kutekeleza programu hii kwa ujumuishi wake na uratibu wa pamoja kwa kuingiza kwenye mipango yetu ikiwa ni wakati muafaka wa maandalizi ya bajeti.

Kitiku pia aliongeza kuwa programu hiyo inategemea sana ushiriki wa Serikali kwa kuweka utekelezaji katika mipango yake na kushirikiana na wadau mbalimbali.

Lengo pia ni kukusanya taarifa kwa kadri inavyowezekana kulingana na viashiria vilivyowekwa kwenye kanzidata na wataalamu hao watafundishwa namna ya kukusanya taarifa na kuziingiza kwenye kanzidata hiyo.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Juma Kaponda, akizungumza kwa niaba ya washiriki, aliishukuru serikali kwa kuanzisha programu hiyo ambayo itasaidia kutoa elimu kwa jamii ili watekeleze majukumu ya malezi kwa watoto.

Kaponda amesema mafunzo hayo yatawajenga na kuwakumbusha umuhimu wa malezi sahihi kwa watoto kwani ni muda mrefu wamekuwa kama wamejisahau. Aidha ameahidi watakwenda kufanya kazi kupitia programu hiyo kwa ufanisi.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya mtoto, imeandaa Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto itakayozunduliwa kesho .

Programu hiyo inatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).



Wachuuzi wakiendelea na shughuli zao juu ya mfereji wa maji ya mvua katika eneo la Goba, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii, bila kujali agizo la Serikali linalowata wafanyabiashara wadogo kutofanya biashara kwenye maeneo yasiyoruhusiwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kanisa laibadilisha jamii mtazamo kuhusu maendeleo

**Na Ashton Balaigwa,**
MORONGORO

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Morogoro kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Makanisa ya Watu wa Norway (NCA - Tanzania) limebadilisha jamii ya vijiji katika kata ya Kilosa kushiriki kikamilifu katika miradi ya kiuchumi ili kuondokana na umaskini.

Mradi huo unaofahamika kama Pima Kadi ya Jamii, umepata mafanikio baada ya wananchi kushiriki kikamilifu kwenye sekta ya elimu na sasa wananchi bila msaada wowote wameweza kutatua tatizo la madawati katika Shule ya Msingi Mandela wilayani Kilosa.

Ofisa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na Uwajibikaji wa Wananchi (CSEE) kutoka Kanisa la Anglikana, Pius Ng'irwa, alisema lengo lake ni kuleta mabadiliko kutoka katika hali ya utegemezi na kuwa na nguvu ya pamoja ya kumaliza changamoto zinazowakabili.

Alisema mradi huo wa miaka mitano utagharimu Sh. milioni 129 kila mwaka na utawezesha kuwajengea uwezo wananchi kuwajibika katika huduma zinazotolewa katika maeneo yao.

Kupitia mradi huo, alisema wananchi wa kijiji cha Mandela walibaini watoto wengi katika shule hiyo wanakaa chini, hivyo baada ya kupewa elimu kupitia mradi huo, walianza kutatua changamoto hiyo kwa kutengeneza madawati 60.

Mratibu wa Miradi hiyo katika wilaya za Kilosa na Mvomero, Boni Mathayo, alisema mwaka 2000 katika kijiji hicho, wananchi walikuwa wakiona miradi yote inayotekelezwa ni mali ya serikali, hivyo hawakuwa wakishiriki.

Alisema moja ya changamoto ilikuwa wanafunzi karibu wote kukaa chini huku wananchi wakidai ni wajibu wa serikali kupeleka madawati hali ambayo ilichangia kufanya vibaya kwa wanafunzi hao.

"Tulipoona hivyo sisi Pima Kadi ya Jamii tuliamua kukaa nao kwa kufanya mikutano kuhusu umuhimu wa wao katika jamii kushiriki kikamilifu kwa kuwa ni faida kwao wenyewe, hivyo kubadilika na kutengeneza madawati kwa nguvu zao wenyewe," alisema Mathayo.

Ofisa Mtendaji wa kata ya Magole, Agnes David, alisema kabla ya kuingia kwa Pima Kadi Jamii, wananchi walikuwa wagumu kujitolea katika shughuli za maendeleo ikiwamo kutatua tatizo la wanafunzi waliokuwa wakikaa chini kutokana na upungufu wa madawati.

Alisema kupitia uhamasishaji wa Pima Kadi Jamii, hivi sasa wananchi kutoka vitongoji vyote vinavyounda kijiji cha Mandela, wanajitokeza pale panapotokea changamoto inayohitaji ushiriki wao, hivyo kuzimaliza na kushukuru mradi wa NCA - Tanzania kwa kuwaletea mradi huo.

Awali, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mandela, Thomas Mpima, alisema shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na tatizo la wanafunzi 226 kukaa chini kutokana na upungufu wa madawati lakini kupitia mradi wa Pima Kadi ya Jamii, limeanza kumalizika.

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo (wa pili kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa mafunzo kwa wawezeshaji kufundisha vijana wa Skauti kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa ulioandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wilayani humo juzi. Wengine ni Kamishina wa Skauti Wilaya ya Muheza, Richard Msagati (kushoto), Mkuu wa TAKUKURU wa wilaya hiyo, Christine Mkango (wa tatu kushoto) na Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma taasisi hiyo wilayani humo, Beatrice Alfred. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Bendera ya TAWA yapeperushwa kilele cha Mlima Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KITENDO cha kishujaa kilichofanywa na Luteni Alexander Donald Gwebe Nyirenda miaka 60 iliyopita katika kilele cha mlima Kilimanjaro (Uhuru Peak) Desemba 9 mwaka huu kilijirudia kwa sura nyingine baada ya askari wahifadhi watano wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kufanikiwa kufika kilele cha mlima mrefu barani Afrika (Kilimanjaro) kwa kuipeperusha bendera ya taasisi hiyo katika kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

TAWA ilishiriki kikamilifu upandaji wa mlima huo uliohusisha taasisi zingine za uhifadhi zikiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Taasisi zingine zilizoshiriki upandaji mlima Kilimanjaro mwaka huu ni pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Lengo la kupanda mlima huo ni kuhamasisha utalii wa ndani kwa kuwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vilivyopo nchini na kuthamini vya kwao.

Askari wahifadhi wa TAWA waliofanikiwa kufika kileleni ni CR III Benson Kamkulu, CR III Renatus Laurent, CR III Mwebeya Nyeura. CR III William Moria na CR III Frank Akyoo, wote wakitokea TAWA Kanda ya Kaskazini.

# EU yapata dawa kukomesha ukatili

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Umoja wa Ulaya nchini, Manifredo Fanti, amesema ukatili wa kijinsia unaweza kupungua kwa kiasi kubwa endapo jamii itashirikiana na serikali na wadau katika kuondoa vitendo hivyo viovu.

Fanti aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, akisema ukatili wa kijinsia siyo jambo la kupuuzwa kwa kuwa linakandamiza uhuru wa watu kupata haki zao katika jamii inayowazunguka. Katika maadhimisho hayo, tuzo mbalimbali zilitolewa kwa wadau na taasisi zilizoshiriki kuunga mkono juhudi za serikali kupinga ukatili wa kijinsia nchini.

Alisema dunia kwa sasa inapambana na tatizo la ukatili wa kijinsia ambao si tatizo la bara la Afrika tu bali ulimwenguni kote.

Balozi huyo alisema jamii inatakiwa kushirikiana na wadau katika kuibua vitendo vya ukatili wa kijinsia ili tatizo hilo lipungue.

Mkuu wa Kitengo cha Ushirikiano na Utamaduni Ubalozi wa Ufaransa, Cecile Frobert, alisema tamasha la hisani la kupinga ukatili wa kijinsia liliambatana na utoaji wa tuzo mbalimbali kwa watu binafsi na taasisi zilizoshiriki katika kutoa mchango wao kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Magharibi Kati Tabora, Dk. Isaac Laiser, ambaye ni miongoni mwa waliopata tuzo hizo, alisema kumekuwapo na tatizo kubwa la utumikishwaji watoto kwenye mashamba ya tumbaku na kusababisha watoto wengi kushindwa kwenda shule.

Alisema tatizo hilo linachangiwa na ugumu wa maisha katika familia zao, hivyo watoto kulazimika kwenda kufanya kazi ili kupata fedha na chakula.

Alisema aliamua kuanzisha programu maalumu ya kuwezesha familia zao kwa kuwapatia mikopo ili wafanye biashara ndogo.

# Jafo akabidhi mpango wa hifadhi na usafi mazingira

**Na Halfan Chusi**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amekabidhi mpango kazi wa kampeni kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira na mwongozo wa Tuzo ya Taifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa wajumbe wa kamati maalumu ya kampeni kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira katika kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mohammed Khamis Abdulla, Jafo alisema lengo la kampeni hiyo ni kuelimisha na kuhamasisha ushiriki wa jamii na uwajibikaji wa mamlaka za usimamizi katika hifadhi na usafi wa mazingira ili kuleta ustawi wa jamii ya Watanzania na maendeleo endelevu.

Katika kufanikisha utekelezaji wa kampeni hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa mpango kazi wa kampeni kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira wa kipindi cha miaka mitano 2021-2026, mwongozo wa Tuzo ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na rasimu ya mkakati wa kutafuta fedha za kuwezesha utekelezaji wa kampeni kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira.

"Nyaraka hizi ni vitendea kazi vya kamati hii maalumu pamoja na jamii ya Watanzania katika utekelezaji wa kampeni hii.

Hivyo ninawakabidhi rasmi nyaraka hizi muhimu kama ishara ya kuwa kazi imeanza rasmi. Niwaombe mtoe uzito wa pekee katika kutekeleza majukumu hayo ya hiari ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo la kampeni," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Kampeni Kabambe, Seif Ally Seif, alisema ni imani yake kuwa utekelezaji wa kampeni hiyo utaanza mara moja na kuwa kamati yake iko tayari kuungana na serikali katika kuwezesha utekelezaji wake kwa ufanisi mkubwa.

Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira ilizinduliwa Juni 5 mwaka huu wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani na Dk. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Tanzania. Kampeni hii itakuwa endelevu na itatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021 hadi 2026.

Wajumbe wa Kamati Maalumu wanatoka katika taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, serikali kuu, mashirika ya umma, mashirika ya kimataifa, asasi zisizo za kiserikali na taasisi za kifedha.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hadhari ya WHO kuhusu corona ipewe kipaumbele

**SHIRIKA** la Afya Duniani (WHO) limetoa tahadhari juu ya ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona nchini hasa katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka kutokana na mikusanyiko ya watu wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Mwakilishi Mkazi wa WHO Tanzania, Dk. Tigest Mengestu, huku akitahadharisha kwamba ugonjwa huo bado upo na unaweza kugharimu maisha ya watu kama hatua za kujikinga hazitachukuliwa.

Kutokana na hali hiyo, Dk Mengestu aliwataka Watanzania kuchukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kuchanja ili kujiweka imara zaidi dhidi ya virusi vya ugonjwa huo, kutokana na taarifa kwamba wimbi la nne limeshaingia katika baadhi ya nchi barani Afrika.

Tahadhari hiyo ya WHO imekuja wakati muafaka kwa sababu kipindi kama hiki, watu wamekuwa wakisafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka. Kutokana mapumziko hayo ambayo hukutanisha ndugu, jamaa na marafiki, watu wamekuwa wakikusanyika na kufanya sherehe mbalimbali.

Licha ya watu wengine kusafiri, wale ambao wamekuwa wanabaki sehemu moja kwa ajili ya mapumziko hayo, pia wamekuwa wakikusanyika kwa ajili ya starehe na burudani, hivyo kuwapo urahisi wa kuambukizana ugonjwa huo.

Sambamba na hilo, WHO imetoa tahadhari hiyo kutokana na hali ilivyojitokeza mwishoni mwa mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu kwa kuwapo ongezeko la ugonjwa huo ambao tangu ulipolipuka umegharimu maisha ya mamilioni ya watu duniani.

Katika mikoa ya kaskazini hasa Kilimanjaro, Arusha na Manyara pamoja na ile ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa, katika kipindi hicho kulikuwa na kasi kubwa ya maambukizi ya corona ambayo ilisababisha watu wengi kuugua na wengine kupoteza maisha.

Pia angalizo hilo ni muhimu kwa sababu idadi kubwa ya watu wameshindwa kufuata miongozo iliyotolewa na serikali juu ya kujikinga na ugonjwa huo. Miongoni mwa miongozo hiyo ni kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kuvaa barakoa, watu kukaa umbali wa mita moja, kuwekwa vyombo vya maji katika sehemu za umma na watu kukaa 'level seat' katika vyombo vya usafiri.

Licha ya serikali kutoa maagizo hayo, kwa kiasi kikubwa hayatekelezwi na watu wamekuwa wakikusanyika kwa wingi katika maeneo mbalimbali bila kuchukua hatua za kujikinga.

Katika vyombo vya usafiri, kwenye viwanja vya michezo na nyumba za ibada, watu wamekuwa hawavai barakoa wala kuchukua hatua madhubuti za kujikinga jambo ambalo ni hatari kwa afa zao na maisha kwa ujumla. Kwenye daladala au mabasi ya kwenda mikoani, unaweza kukuta watu wawili au watatu tu waliovaa barakoa huku wengine wakiwa hawajavaa.

Ni vyema Watanzania, kama ilivyotahadharisha WHO, kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka vinginevyo tunaweza kushuhudia vifo vitokanavyo na changamoto ya kupumua kama ilivyokuwa mwanzoni mwa mwaka huu.

Kama wahenga wasemavyo kinga ni bora kuliko tiba, kila Mtanzania achukue tahadhari kujikinga na ugonjwa huo. Sambamba na kujikinga kwa kufuata miongozo ya serikali, ni vyema watu wakaendelea kupata chanjo ya ugonjwa huo ili kupunguza uwezekano wa kuambukizwa au kupata madhara makubwa pindi mtu atakapokumbwa nao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Masoko machinga yakiboreshwa kadhia hii inaweza kumalizika

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** inahamisha wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, kutoka katika maeneo ya awali yasiyo rasmi waliyokuwa wakiyatumia kufanyia biashara zao, ili kwenda katika masoko ambayo wamejengewa.

Pamoja na nia njema ya serikali, kumekuwapo na sintofahamu katika baadhi ya maeneo kutokana na kwamba baadhi ya machinga waliohamishwa, wakati wa jioni wanarudi kule walikoondolewa na kuendelea na biashara.

Sababu ya kuwatoa katika masoko wakati wa jioni ni kwamba hakuna biashara, hivyo wanaona ni bora wawe wanarudi kandokando ya barabara kuendelea na biashara angalau wapate chochote.

Mbali na sababu hiyo, nyingine ni kwamba katika masoko waliyotengewa hakuna miundombinu ya muhimu kama usafiri, maji na huduma nyingine, hivyo kuendelea kushinda katika masoko hayo ni kujiumiza.

Kwa wale wanaofuatilia sakata la wafanyabiashara hao, watakumbuka kuwa madai yao si ya leo wala jana, bali ni ya muda mrefu na yalisababisha Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli (sasa marehemu) kuagiza uboreshaji wa masoko.

Kwa kuwa malalamiko yao ni yale yale, ni vyema manispaa na halmashauri nchini zikatoa ufafanuzi ili jamii ijue ukweli ni upi, na kama kile wanachosema kina ukweli, basi masoko yaboreshwe.

Wakati huu ambao machinga wanahamishwa, ingependeza kama viongozi wa halmashauri na manispaa wakafanyia kazi malalamiko hayo na kuyapatia ufumbuzi ili kuepusha adha ya kuzunguka na bidhaa zao huku na kule.

Ninaamini kwamba njia mojawapo ya kuwafanya watulie sehemu moja, ni kuwaboreshea masoko

**Wakati huu ambao machinga wanahamishwa, ingependeza kama viongozi wa halmashauri na manispaa wakafanyia kazi malalamiko hayo na kuyapatia ufumbuzi ili kuepusha adha ya kuzunguka na bidhaa zao huku na kule.**

ili wafanye biashara na kunufaika nayo, lakini pia kuwaepusha na ajali na uchafuzi wa mazingira.

Ikumbukwe kuwa baadhi yao wamekuwa wakifanyia biashara katika maeneo hatarishi, ikiwamo kando ya barabara hali ambayo wanaweza kugongwa na magari na wengine chini ya nyaya za umeme mkubwa.

Mazingira hayo kwa ujumla si salama, lakini baadhi yao huwa wanasema hawana jinsi, na kwamba hata kama si salama, ni bora wafanyie tu katika maeneo hayo ili mradi mkono uende kinywani.

Kwa kuwa viongozi wa halmashauri na manispaa wapo na wanaona jinsi machinga wanavyozunguka huku na kule kujitafutia riziki hata kwenye mazingira hatarishi ni bora hatua za kuwasaidia zikachukuliwa haraka.

Ipo mifano mingi, lakini mmojawapo ni wa machinga wa Mbezi mwisho, Dar es Salaam, ambao wakati wa asubuhi hadi saa kumi jioni huwa hawaonekani kwenye maeneo waliyoondolewa, lakini kuanzia saa 11 huwa wanarudi.

Hiyo nenda rudi na mizigo mabegani kila siku ni kero, ni vyema uchunguzi ukafanyika kubaini sababu za kurudi wakati wa jioni, kama zina ukweli, basi zitafutiwe ufumbuzi iwapo ni mazoea tu, wasaidiwe kuachana na mtindo huo.

Kuondolewa kwa machinga katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, kumeanza kuonyesha mandhari nzuri ya jiji hilo na uasilia wake, kwa kuwa maeneo ambayo awali yalitumiwa na machinga, sasa yako wazi.

Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza machinga wapangwe vizuri, sasa wanapopangwa vizuri kisha wanarudi katika maeneo waliyoondolewa, hiyo inaonyesha kuwa kuna jambo halijakaa sawa.

Tatizo linaweza kuwa ni la machinga wenyewe au viongozi wa mamlaka husika, hivyo ni vyema kila upande ukaangalia ni wapi umekosea ili kuweka mambo sawa kwa kuepusha nenda rudi

SAFU/MAKALA

KWA MASLAHI YA TAIFA

# Bila wajasiriamali kusaidiwa AfCFTA, ni wazi Tanzania tutakuwa watazamaji



Na Pascal Mayalla

Ni mpaka nilipohudhuria haya maonyesho ya Mwanza yaliyohusisha wajasiliamali kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na wenyeji Tanzania kuna jambo nimejifunza.

KWA takriban siku 10, nimepiga kambi jijini Mwanza katika viunga vya Rock City Mall kuhudhuria maonyesho ya wajasiriamali wadogo na wa kati wa nchi sita za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, maarufu kama Maonyesho ya Jua Kali.

Siku zote unapokuwa peke yako, huna mtu wa kujilinganisha naye. Unaweza ukajiona wewe ni bingwa. Mfano ukiingia ulingoni, peke yako, hakuna mpinzani wa kupigana naye, ukatupa ngumi kwenye upepo, utajiona ni bingwa. Au mechi za mpira za ligi kuu, timu moja ikiingia uwanjani, timu pinzani ikatia mpira kwapani, ile timu iliyoingiza timu uwanjani, inakula pointi tatu za bure za ushindi wa mezani.

Ili ujijue ubora wako na uimara wako ni pale unapopata ushindani. Siku zote nimekuwa nikihudhuria maonyesho mbalimbali yanayohusisha wajasiriamali wadogo na wa kati wa nchini mwetu kupitia maonyesho mbalimbali yakiwamo Sabasaba na Nanenane. Katika maonyesho hayo, nimeshuhudia bidhaa za wajasiriamali wa Tanzania zikizidi kuboreka.

Ni mpaka nilipohudhuria haya maonyesho ya Mwanza yaliyohusisha wajasiriamali kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na wenyeji Tanzania kuna jambo nimejifunza.

Ukifanya ulinganifu wa bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati wa Tanzania na baadhi ya nchi, kumung'unya maneno, Watanzania ni kama tunacheza. Maonyesho kufanyika katika nchi yetu, ilitarajiwa wajasiriamali wa Tanzania ndio wayatawale kwa wingi wa bidhaa za Tanzania, lakini hali si hivyo!

Watanzania ndani ya viwanja hivi tumekuwa kama wageni, halafu wageni ndio wametamalaki kwa bidhaa bora na nyingi kuliko wenyeji. Wageni ndio wanatamba, huku wenyeji tumenyong'onyea.

Kwa kutumia taaluma yangu ya uandishi wa habari nikaamua kufanya uandishi wa kiuchunguzi, kufanya inteligensia ya kibiashara, nchi ndogo na masikini kuliko Tanzania, zimeweza vipi kuleta wajasiriamali wengi na kuleta bidhaa nyingi hadi mabanda waliyopangwa hayatoshi. Bidhaa zimefurika hadi kupangwa barabarani.

Katika uchunguzi huo, ndipo nilipobaini wajasiriamali wa nchi za wenzetu, wanasaidiwa na serikali zao kuanzia chakula, malazi, usafiri na kupewa fedha za kujikimu. Hiyo imesaidia kuleta mafurushi ya bidhaa huku wajasiriamali wa Tanzania, wakiachwa kujibeba kwa kauli ya "pambana na hali yako".

Sasa kama serikali yetu haitawasaidia wajasiriamali wetu wadogo na mfano mzuri ni jinsi Watanzania na bidhaa za Tanzania kusuasua katika masoko huru ya Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika kunakosababisha bidhaa za baadhi ya majirani kutamba, hali itakuwaje kwa soko huria la AfCFTA?

Serikali ikiwaachia sekta binafsi wajibebe, kiukweli katika soko la AfCFTA, Watanzania tutaishia kuwa Watazamaji!.

Serikali yetu iko makini sana katika kukusanya kodi, hivyo kila bidhaa inayozalishwa nchini, lazima itozwe kodi. Baadhi ya majirani zetu, ili kuingiza bidhaa zao masoko ya kimataifa, wanaondoa kodi zote kwenye bidhaa zinazouzwa nje. Ndiyo maana kwa mikoa ya pembezoni, mfuko wa sementi wa Tanzania umefika Sh. 24,000 wakati sementi ya jirani mpaka inafika sokoni ni Sh. 12,000. Hii inawezekana kwa sababu serikali zao zinatoza kodi sifuri.

Wajasiriamali wadogo na wa kati wa Tanzania, wanajitahidi kuzalisha bidhaa bora na vifungashio bora na zina nembo za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na barcode. Lakini hawawezi kupeleka bidhaa zao kwenye maonyesho ya kimataifa bila kushikwa mkono.

Kuna wakati New York, Marekani kulifanyika maonyesho ya utalii katika hoteli ya Inter Continental New York. Niliposikia Tanzania inashiriki, nikiwa Mtanzania mzalendo, nilikwenda kuangalia. Kiukweli niliona aibu. Tanzania ilikuwa na banda moja tuu la Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) wakati jirani zetu, walikuwa na mabanda 18.

Ukifuatilia urari wa biashara na bidhaa katika soko la AGOA kutoka Tanzania, ukilinganisha na majirani zetu, utashangaa. Tanzania ni kama tumelala. Hata baadhi ya bidhaa kutoka nchi jirani, zinazoingia kwenye masoko ya kimataifa ni zetu. Mpaka kesho, Tanzania ndiyo nchi pekee inayozalisha madini ya Tanzanite lakini katika masoko ya kimataifa, India ndiyo inayoongoza, ikifuatiwa na Afika Kusini na Kenya. Tanzania ni ya nne!

Kwenye Maonyesho ya Jua Kali hapa Rock City, nimehesabu mabanda ya kila nchi. Maonyesho yameanza Desemba 2 na yanamalizika leo lakini niliwaona mawaziri wetu wawili tu, Jenista Mhagama Desemba 4 (Tanzania Day), na Waziri wa Viwanda na Biashara Prof. Kitila Mkumbo aliyekuwa mgeni rasmi ile siku ya ufunguzi Desemba 5.

Hali ikiwa hivyo, nchi moja ya jirani kila siku ni waziri mmoja anatembelea, wakurugenzi wote wa taasisi zao, wamepiga kambi hapa Mwanza.

**Itaendelea...**

**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tembo Warriors nao wapewe udaktari wa heshima



Na Joseph Kulangwa

Hii ni shahada ya 'Udaktari wa Heshima', wanaiita 'Honoris Causa' wenye nayo kwamba mchango wako katika jamii, ndio unasababisha utambulike. Inawezekana Musukuma katambuliwa na waliompa kwa kuwasiliana na watu wa Geita Vijijini.

HAKUNA binadamu mwenye akili katika sayari yoyote anayekubali kushindwa au hata kudharaulika. Ni vivyo hivyo hata kwa wanyama. Ndiyo sababu hutokea ugomvi baina ya mtu na mtu au mnyama na mwingine.

Hapo hutokea mmoja anataka kumzidi mwingine, iwe kwa ufahari au kwa majigambo tu na kutaka kuonekana fulani ndiye yeye katika jamii na kusifiwa na kuvimba kichwa, hivyo ni bora kukubaliana, kinyume cha hapo ni mtafaruku.

Watu hupenda kusoma ili kupata maisha mazuri. Hakuna asiyelijua hilo na hakuna anayelikataa. Na maisha mazuri hayo ndiyo humfanya ashindane na mwingine ndiyo maana watu hutaka kuigana kimaisha. Asiye nacho hutaka kumwiga aliye nacho.

Ushindani huo wa kuigana, wakati mwingine usiposababisha mtafaruku husisan kutoka kwa mwenye nacho, asiyetaka asiye nacho amfikie lakini mambo yakiwa shwari hujikuta pande mbili zikachipuka na kujikuta ziko juu.

Wasomi wengi hupenda kusoma mpaka kupata shahada za juu ambazo ni za uzamivu ili tu kuitana dokta fulani au hata Profesa fulani. Hapo ndipo hujiona kafika kileleni mwa maisha ya kisomi.

Na hilo hakuna abishaye kuwa ni jambo jema kwa maisha ya binadamu na kwa jamii kwa ujumla. Wanyama hawasomi, wanyama hawahitaji udaktari au uprofesa lakini hupenda kujigamba kwa mabavu waliyo nayo, hususan wale wa kiume.

Hivi karibuni nchini kuliibuka tukio la Mheshimiwa Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku a.k.a. Musukuma, aliyepata alichosema ni Shahada ya Uzamivu (PhD) bila shaka katika uongozi nadhani na siasa!

Musukuma alitamba sana kwenye mitandao ya kijamii na kusema kuanzia sasa aheshimike kuwa ni Daktari akihanikiza kuwa mwenye PhD, aliyopewa na chuo sijui kutoka India nadhani. Akafikia hatua ya kusema wasimwonee wivu kwani sasa ni matawi.

Akasema hivi sasa ana uwezo hata wa kupatanisha mataifa makubwa yaliyo kwenye mzozo kwa sababu sasa ni mtu wa PhD. Sikumwelewa lakini nikamkubalia kuwa anaweza kwa sababu kupatanisha ni maneno unayoweza kuyatoa ukakubaliwa na pande mbili kama zitakuelewa katika uwasilishaji wako.

Hii ni shahada ya 'Udaktari wa Heshima', wanaiita 'Honoris Causa' wenye nayo kwamba mchango wako katika jamii, ndio unasababisha utambulike. Inawezekana Musukuma katambuliwa na waliompa kwa kuwasiliana na watu wa Geita Vijijini.

Nampongeza kwamba ametambulika sana kutokana na shahada hiyo hasa ikizingatiwa kuwa ni darasa la saba aliyeruka koote huko mpaka kupata Udaktari wa Heshima. Naye kwa tambo zake lazima ajulikane hasa kutokana na alivyokuwa akibeza wasomi bungeni.

Sina tatizo naye kabisa. Hongera Dk Musukuma. Nimekuwa nikifanya hivi hata kwa marehemu Dk. Remmy na hata kwa Profesa Maji Marefu na wengineo waliozipata kwa michango yao katika jamii. Hili liendelee tu hata kwa wengine ili hatimaye tuwe na madaktari wengi nchi hii na tuonekane tumeendelea.

Bila shaka kwa mwendo huu na mwingine na tukiongeza madaktari, sasa hivi tutahama uchumi wa kati wa chini na kufikia uchumi wa kati wa juu. Mashallaah Mungu atupe nini sasa!

Basi kwa hili nawasilisha ombi langu kwenu wadau, kutambua kuwa wachezaji wa timu ya Taifa ya Wanaume ya Soka la Walemavu Tembo Warriors ndio madaktari wangu. Natangaza kuwapa udaktari wa heshima kuanzia sasa, kwa walichokifanya.

Watu hawa wametufikisha kwenye fainali za Kombe la Dunia, mwakani tutakutana na mataifa mengine ya huko mbali nchini Uturuki, kuwania kombe hilo, na inawezekana wakalitwaa na kuzidi kuiinua Tanzania katika medani hiyo ya michezo.

Kama hili litakubalika, basi na iwe hivyo na tulinganishe mchango wake na huo wa kina Musukuma na shahada kutoka India. Nadhani ya kwetu hii itakayokuwa imetolewa na Watanzania karibu milioni 60 itakuwa na uzito mkubwa kwa sababu mchango wao ni dhahiri. Au mnasemaje?

**Alamsiki!**

## SAFU

## KONA YA UKWELI

# Mafanikio makubwa yamefikiwa miaka 60 ya uhuru, tusibeze



Na Thobias Mwanakatwe

SAA 3:00 usiku Desemba 8, mwaka huu, nilikuwa makini kusikiliza hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan wakati akizungumza na Watanzania kupitia vyombo vya habari.

Mara tu baada ya kutolewa taarifa kuwa Rais atazungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari, kama ilivyo kwa wabongo kwenye mitandao ya kijamii, watu wakaanza kutabiri mambo ambayo wanadhani atayazungumza.

Katika utabiri huo, wako waliosema Rais angetumia mamlaka yake kisheria kutangaza kumuachia Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, anayekabiliwa na kesi ya ugaidi. Kimsingi baada ya kusoma utabiri huo nilicheka kidogo.

Ulipofika wakati uliosubiriwa, nikaweka runinga na kuanza kumsikiliza Rais. Kimsingi, hotuba yake ilikuwa nzuri kwani ilijikita kuelezea mafanikio yaliyopatikana baada ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 60 sasa baada ya Uhuru.

Rais alitaja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni wastani wa pato kwa mtu kwa mwaka 1961 lilikuwa Sh. 776 na kwa mwaka 2020 ni Sh. 2,653,790. Jambo hili limeongeza hadhi yetu machoni pa jumuiya ya kimataifa na kutuondolea unyonge.

Akasema kutokana na kukua kwa uchumi katika nchi yetu, usafiri wa anga si suala la anasa, hivyo kufufuliwa au kuimarishwa kwa Shirila la Ndege Tanzania (ATCL) ni jambo la lazima. Tumeshanunua ndege 12 na malipo ya ndege zingine tano yameshafanyika.

Tanzania inakadiriwa kuwa na zaidi ya makabila 120. Pamoja na tofauti zote hizo, tumekuwa na taifa moja na kuunganishwa na lugha ya Kiswahili. Si kitu rahisi. Katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, tumefikia uchumi wa kati mapema hata kabla ya lengo la kufikia hatua hiyo mwaka 2025. Hali hii inatuondolea unyonge kimataifa na kutuondolea unyanyapaa.

Tumeunganisha mikoa kwa barabara za lami na kazi ya kuunganisha makao makuu ya wilaya kwa barabara inaendelea. Wakati tunapata uhuru tulikuwa na meli sita na sasa tuna meli 14 zinazofanya kazi katika Ziwa Nyasa, Victoria na Tanganyika.

Wakati tunapata uhuru nchi yetu ilikuwa inazalisha megawati za umeme 17.5 tu, lakini sasa tunazalisha megawati 1,909 huku tukiwa na matarajio ya kuongeza megawati zingine 2,115 litakapokamilika kujengwa bwawa la Nyerere [JNHPP].

Kwa upande wa elimu, wakati tunapata uhuru tulikuwa na walimu wa shule za msingi 36 lakini sasa tuna walimu wa ngazi hiyo 281,728. Pia tumepiga hatua kwenye eneo la elimu ya juu kwani kwa sasa tuna vyuo vikuu 30 vya serikali 18 na 12 vya sekta binafsi na vyuo vikuu vishiriki 17.

Kilicho dhahiri katika sekta ya afya ni ule uwezo wa kutoa huduma za kibingwa ambazo zamani hazikuwapo na tulikuwa tukilazimika kupeleka wagonjwa nje ya nchi na hivyo kutumia fedha nyingi za kigeni.

Umri wa kuishi kwa Watanzania umeongezeka kutokana na uboreshaji na upatikanaji wa lishe na kuondoa udumavu. Wakati tunapata uhuru wastani wa umri wa kuishi kwa Watanzania ulikuwa miaka 37 na sasa ni miaka 67.

Tanzania imeendelea kuimarika, nguvu ya kushawishi imeendelea kukua na kuaminika ikiwamo Watanzania kuongoza taasisi mbalimbali za kimataifa. Tulikuwa na balozi mbili tu mwaka 1961 na sasa tuna balozi 44. Diplomasia yetu inapanuka na inaendelea kung'ara duniani.

Tangu kurejea kwa mfumo wa vyama vingi tuna vyama vilivyosajiliwa 19 na 17 vinavyoomba usajili wa muda na tumekuwa na mfumo bora na imara wa kuweka viongozi madarakani ambao unaheshimiwa na kuaminiwa.

Tumekuwa na mfumo imara wa utoaji haki kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia msingi wa kuwa binadamu wote ni sawa na hakuna aliye juu ya sheria.

Tutunze mazingira yetu kwa uchungu mkubwa ili turithishe kwa watoto na vizazi vyetu nchi ambayo ni ya neema kama ilivyokuwa kwetu.

Dira yetu ya maendeleo kufikia 2025 inaelekea kumalizika ambapo tunatarajia kukua kwa uchumi kwa asilimia nane. Tunapoangalia mbele tunakwenda kuandaa dira ya miaka 25 ijayo (2025-2050) ambayo itaelekeza kukua kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Rais akasisitiza kuwa mafanikio tuliyoyapata kwa miaka 60 yamebebwa na utawala wa sheria na utawala bora. Tumekuwa na mfumo bora unaoheshimiwa wa kuweka viongozi madarakani kupitia chaguzi zinazofanyika kila baada ya miaka mitano.

Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna baadhi ya watu wanabeza kuwa hakuna kilichofanyika kana kwwmba bado tupo pale pale wakati kiukweli tumepiga hatua kubwa kimaendeleo.

Natambua kuwa si rahisi kumaliza changamoto zote maana hata katika nchi zilizoendelea changamoto bado hazijaisha. Hivyo wakati umefika kwa Watanzania kutambua kuwa maendeleo makubwa yamefanyika nchini.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Mungu Ibariki Afrika**

## DARASA LA NDOA

# KUINGILIA NDOA ZA WATOTO NI SUMU



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

NDOA ni taasisi ya kwanza ya kijamii na takatifu iliyoanzishwa na Mungu na yenye mamlaka na utawala kamili. Wazazi wengi wamesahau kuwa ndoa ni taasisi huru inayojitegemea.

Uzoefu unaeonesha kuwa baadhi ya wazazi na ndugu huchangia kuvurugika na kuvunjika kwa ndoa za watoto wao badala ya kusaidia kuzidumisha. Mtu anaweza kuwa na ndugu lakini si kila ndugu anakuwazia na kuitakia ndoa yako mema.

Katika ndoa kuna kanuni tatu ambazo wanandoa, wazazi na ndugu wanapaswa kuzingatia. Kanuni hizo ni kuacha, kuambatana na kuwa wamoja.

**Kuacha**

Kuacha kuna maana zaidi ya kuondoka na kwenda kuishi mahali pengine na mke au mume. Kuacha kunamaanisha kuwa tangu siku ya harusi, uhusiano wa mwanamume na wazazi au ndugu zake unapunguzwa na uhusiano mkubwa utakuwa na mke au mume wake.

Neno kuacha linaonyesha sababu, umuhimu na maana ya mwanamke kwa mwanaume, kutokana na mpango wa Mungu wa uumbaji. Neno kuacha linabadili uhusiano wa kibinadamu uliozoeleka kabla ya ndoa.

Hii ina maana kwamba mwanaume anapooa, uhusiano wake na mkewe ni jambo la msingi na kipaumbele cha kwanza. Kwa msingi huo, vijana wanapoandaliwa kuingia katika maisha ya ndoa wanahitaji kuandaliwa kisaikolojia kukabili badiliko hili.

Kwa mantiki hiyo, vijana waandaliwe kuondoka, kujitegemea na kuwa na uhuru wa kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa. Aidha, Wazazi wao nao wanahitaji kufahamu badiliko hili muhimu.

Katika kuacha, kunajengwa familia mpya, ambapo wanandoa wanahitaji kujenga utambulisho wao, hivyo, kujitenga kwa kiasi fulani, kutoka kwa wazazi kimwili, kihisia, kiufahamu, kimaamuzi na kimapato.

Wanapaswa kuwa na uhuru na faragha binafsi, uhuru katika kufikiri mambo yenye faida kwao wawili na ndoa yao, uhuru katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu maisha yao na wazazi wao au ndugu zao, uhuru katika mapato yao na matumizi yake kwa ustawi wa familia yao.

Wanandoa wanakuwa na mamlaka na utawala kamili. Kwa hiyo, Wanandoa kuendelea kuwa tegemezi kwa wazazi wao, kuishi kwa mashinikizo na kuongozwa na watu wengine ni dalili ya kutokukua. Hali hii huondoa uhuru na kujiamini kwa wanandoa katika kuendesha na kusimamia maisha yao ya ndoa.

Mtu akiwa ameoa au kuolewa maana yake ni kwamba, amekuwa mtu mzima mwenye maamuzi. Hivyo, mwanandoa kusubiri kuambiwa afanye nini au kufuata kila kitu wazazi au ndugu wanachotaka au wasichotaka, ni kuikosea ndoa na matokeo yake ni misuguano na ugomvi ndani ya ndoa, kwani nafasi ya mwenzi inakuwa haipo tena.

Baba au Mama, kaka au dada wanastahili kuheshimiwa nasi kama binadamu kwanza, halafu kama ndugu au wazazi. Lakini, kuwa ndugu au wazazi hakuwapi watu hawa haki na mamlaka ya kuingilia ndoa ya watoto wao au ndugu zao.

Pamoja na kwamba mtoto hakui kwa mzazi, lakini inapofikia hatua ya ndoa, kuna mipaka ya kutunzwa na kuheshimiwa na wazazi ili ndoa ikue. Kukua ni pamoja na kujua kwamba, hata mzazi anaweza kukosea kama binadamu mwingine yoyote.

Ni vema ifahamike kuwa, Kuacha haimaanishi kutelekeza au kuondoa nafasi ya wazazi kwa watoto wao, bali kutoa uhuru kwa watoto wao walioana kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kupokea amri kutoka kwa wazazi.

Kufanya hivyo ni sehemu ya kuheshimu mipaka na ndoa ya watoto wao na kutambua kuwa, sasa ni watu wazima wenye uwezo wa kufanya maamuzi na wenye majukumu mapya.

Wazazi wanaweza kutoa ushauri pale unapohitajika na sio kutoa amri. Kama ushauri unakusudia kujenga na kuimarisha maisha ya ndoa ya watoto wao badala ya kuwavuruga, unaweza kupokelewa.

Wanandoa kama watu wazima, wanao wajibu wa kupima kila ushauri unaotolewa au maneno wanayoelezwa na mtu yeyote yule, kwani wakati mwingine ndoa huvurugwa na ndugu, wazazi, marafiki, majirani, wafanyakazi wenzetu, yamkini hata wale tunaoabudu pamoja nao. Kumbuka, mara nyingi watu wanaoweza kukuumiza huwa hawatoki mbali, mara nyingi huwa ni wale walio karibu nawe.

Baadhi ya wazazi wamekuwa waamuzi wa maisha ya watoto wao katika ndoa. Mzazi anaweza hata kumpangia mwanaye ampe fedha kiasi fulani kila mwezi kwa sababu tu yeye ni mzazi. Mzazi anaweza kumpangia mtoto aishi vipi na mkewe au mumewe, awalee vipi watoto wake na masuala mengine ya kimaisha.

Hapa si tu kwamba, wazazi hawa wanaweza kwa kadiri wawezavyo kuwaingilia watoto wao kwenye ndoa zao, bali huwafanya watoto wao kushindwa kukua na kuwa tegemezi. Wanandoa wanawekwa katika hali ya kuamini kwamba, mzazi ndiye mwenye haki ya kumsemea kuhusu maisha yake kuliko haki yake mwanandoa mwenyewe.

Wanandoa wasioruhusiwa kukua na kujitegemea, huwa hawako tayari kwenda kinyume na utashi wa wazazi au ndugu, hata kama wanauona utashi huo ni kinyume na matakwa yao.

Hawaamini kamwe kwamba wana haki ya kuamua kuhusu maisha yao kama binadamu kamili. Kwa bahati mbaya nao wanaweza kuja kuwatendea watoto wao hivyo na watoto hao wakaishi bila kukua kwenye uhusiano. Ndipo unapojengwa ukoo wa wazazi au ndugu wenye kuingilia ndoa na vivuruge.

Kutokana na wazazi au ndugu kuwa katika umaskini wa kimapato, kunaweza kuwa na utegemezi kwa mtoto wao. Kama tujuavyo, mtu anapooa huanza kuelekeza nguvu nyingi kwenye ndoa au familia yake, badala ya nyumbani.

Kutokana na hali hiyo, ndugu au wazazi wa mume wanaweza kudhani kwamba, mke wa mtoto wao au ndugu yao ndiye chanzo cha misaada kupungua au kusimama. Umakini na kujitambua kunahitajika sana katika mambo haya.

**Itaendelea Jumapili Ijayo**

■**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

DESEMBA 12, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

**PUNGUZA UZITO**

**Kwa juisi ya tango**



Ukurasa 15

## NYUMBA:

Jifunze namna ya kusafisha sofa


12 MAISHA JUMAPILI DESEMBA 12, 2021

HARUSI

Novemba 27 mwaka huu Phinias Matunda au 'Phinmat

HARUSI

Ukurasa 12




## KARABATI NGOZI

# Tango, nyanya, asali vinatosha kukupa furaha

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | A | N | D | E |
| ■ | E | ■ | ■ | O | ■ |
| I | P | O | ■ | D | ■ |
| ■ | O | ■ | D | O | A |
| ■ | N | ■ | ■ | M | ■ |
| T | I | M | B | A | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMO, PAA, KAMBI, JUMBA, JAMBIA, BOMANI

## WATOTO

# PAKA RANGI




MTOTO Karim alikwenda sokoni kununua mboga, alipofika katika eneo la kuuzia samaki aliona mchuuzi akiwaondoa samaki walioharibika huku harufu kali ikitawala eneo hilo.

Baada ya kuona hali hiyo, Karimu alimfuata yule mchuuzi na kuanza kumuuliza.

Karim: Hawa samaki unaowaondoa wamefanya nini?


Mchuuzi: hawa wameharibika nawaweka pembeni ili niwatupe dampo

Karim: Lakini si nasikia samaki akioza mmoja, wote wanakuwa wameharibika?

Mchuuzi: Hapana mtoto, huo ni msemo tu kuna samaki wazima na hawatoi harufu, bali wanaosema hivyo wanatahadharisha tu kwamba unapofanya ubaya basi wakaribu yako nao watahusishwa.

SWALI

Mnyama Kiboko anaishi katika maji ya mito na maziwa, je anapotaka kula anakwenda wapi?




Alichokifanya Adaktari

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Jaribu lako lisikutoe kwenye ndoto ya mafanikio yako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu. Bila shaka umenufaika na mada zilizopita zikiwemo vita katika nafasi au cheo chako. Leo nijikite kwenye vita vya jaribu lako.

Tunaposema jaribu, hakuna mwanadamu mwenye akili timamu ambaye hajui maana ya jaribu. Au hakuna ambaye hajawahi kupitia jaribu lililomtikisa katika maisha yake.

Kwa tafsiri nyepesi, jaribu ni changamoto inayoleta mtikisiko kwa mjaribiwa, yaani yule anayepatwa nalo. Lakini pia katika jaribu kuna vita. Unaweza kuwa kwenye jaribu ukakumbana na vita fulani.

Wako wengi wamepotelea na kufa katika majaribu. Hii ikimaanisha kuwa yuko kwenye jaribu, kisha inainuka vita kwenye jaribu lake, naye anapotelea na kufia huko. Watu wengi hawataki majaribu, wanakimbia majaribu.

Lakini pia wengine wamedhani kujaribiwa kwa mtu kunatokana na kutenda dhambi. Mtu anapokutana na jaribu fulani, basi wanajua ya kwamba huyu ametenda dhambi ndio maana anakumbana na changamoto hii.

Msomaji wangu, ni kweli kwamba jaribu linachoma kama moto. Lina maumivu makali, linatengeneza ukuta ambao unakufanya usione ng'ambo yako. Kuna msemo kwamba tumesamehewa dhambi lakini si majaribu.

Mtu mwingine akasema, majaribu ni mtaji. Hata kama wewe ni mtumishi wa ngazi gani, lakini ni lazima jaribu ukutane nalo. Katika eneo lolote lile, yawezekana ni jaribu la ndoa, jaribu la mtoto, afya au uchumi.

Mungu ameweka wazi suala la majaribu pale aliposema: "Kwa hiyo ajidhaniaye amesimama, na aangalie asianguke. Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya mlango wa kutokea ili mweze kustahimili.

Yaani jaribu lililokupata si zito kupita vile unavyoweza. Pamoja na jaribu ambalo limekuwa changamoto kubwa kwako au giza, au ukuta mbele yako, Mungu atafanya mlango wa kutokea.

Hata katika majaribu na maumivu uliyo nayo au uonevu juu yako, Mungu hatakuacha uteketee, maana atatengeneza au atasababisha namna utakavyoweza kutoka kwenye hilo jaribu. Ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke. Asitambe eti mimi sijaribiwi awe ni mkurugenzi au wa cheo chochote kile. Majaribu ni sehemu ya maisha yetu!

Lakini ni muhimu uliangalie jaribu litakalokuja lisikufanye ukaanguka, ukakimbia. Ukaona eti kwamba hili jaribu ni nzito sana. Ukiona hili jaribu si la kawaida bali ni tofauti, Mungu anasema; Hatatuacha tukajaribiwa vile ambavyo hatuwezi.

Msomaji wangu, unaweza kumuona jirani yako anapitia magumu fulani, pengine mumewe anampiga mara kwa mara baada ya kurejea akiwa mlevi. Wewe unachekelea badala ya kumhurumia na kumshauri mama mwenzio umtie moyo. Hilo ni jaribu lake, wewe je? Hata kama hujalipata, linakuja!

Ni rahisi kufuatilia jaribu la mwenzako, kumbe lako lipo njiani linakuja. Ni rahisi kulinganisha jaribu lako na mwingine, kwamba la kwangu ni zito kuliko huyu. Lakini kumbe kila mtu ana kujaribiwa kwake, kwa wakati wake, ana maumivu yake na katika muda wake.

Jaribu linaweza kumng'oa ambaye kwa macho hutaamini kwamba anaweza kutikiswa. Wengi wameshindwa kustahimili, wamepoteza furaha zao, wameibiwa amani zao, maamuzi yaliyo sahihi yametekwa sababu ya majaribu.

Watu wamebadilishwa misimamo kwa kujaribiwa. Familia zimefarakana kwa sababu ya majaribu. Usimdhihaki mtu wakati wa kujaribiwa kwake, hujui maumivu yake wala hujiu aibu yake.

Mbaya ni wakati wa jaribu inapokuja vita. Wapo wanaotamani upotelee katika jaribu hilo.Mfano mama aliyechelewa kupata mtoto kwenye ndoa. Yupo katika jaribu halafu inainuka vita. Akimtuma mtoto wa jirani anaambiwa, "zaa na wewe umtume".

Maneno kibao upande wa mume; Unamaliza ugali wa kaka yetu. Wapo waliochelewa kuzaa wakaachika. Mmoja aliolewa akadumu miaka 15 bila mtoto. Mama mkwe alipokuwa anamtembelea anachukua jagi la maji anafungia mgongoni, anaanza kubembeleza kama mtoto.

Akiulizwa, anajibu, "huyu ndiye mjukuu wangu katika hii nyumba. Hutaki hivi, basi ungezaa!" Siku nyingine anakuja na vijinguo vya mtoto. Anavalisha jagi anafungia mgongoni. Jiulize, dada huyu alikuwa katika maumivu ya aina gani? Acha wachochee vita wanakutengenezea njia, kwani kila jaribu lina mlango wa kutokea!

Niishie hapa. Bila shaka umejifunza kitu hapo. Majaribu hayana budi kuja, lakini tutayashinda yote. Je, una maoni, kisa?

***Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Taa hizi za barabarani zinatumika kuumiza madereva

UNAPOENDESHA gari kwenda Posta kutokea Morocco lazima upite kwenye taa saba ambazo zote lazima ufuate utaratibu wa kusimama na zikishakuruhusu ndipo uendelee na safari yako.

Taa hizo ni za Morocco ambako kuna matengenezo ya barabara yanayoendelea na mara nyingi kuna askari wa usalama barabarani wanaoongoza magari. Mara chache taa hizi zinatumika na haziwaki vyema.

Ukishavuka taa hizo, kuna taa za Namanga ambazo kama ilivyo kawaida ni lazima usimame uruhusiwe ndipo uendelee na safari.

Nazo zinawaka kwa taabu na zimefifia. Ukisogea mbele kuna taa za Mbuyuni ambazo kama ilivyo kawaida ya sheria za usalama barabarani lazima usimame tena, ikishakuruhusu ndipo uendelee na safari.

Ukiendelea na safari, utakutana tena na taa za Ubalozi na mbele kuna taa za Selander na zingine za Serena. Zote hizo zimechakaa kiasi cha kuwa mtaji kwa askari wa usalama barabarani.

Kati ya zote, zilizo taabani zaidi ni za Namanga na Mbuyuni ambazo wakati mwingine huwasha taa ya njano wakati inatakiwa kuwa kijani ili kuruhusu magari kupita, jambo ambalo linawachanganya madereva.

Pia taa inayoruhusu magari kwenda Msasani haiwaki, inatumika nyingine na ikiwa dereva atapita basi polisi huwa wamejificha eneo fulani kwa ajili ya kukamata magari kwa madai wamepita kwenye taa nyekundu.

Zingine ni za Mbuyuni. Ukiwa unatokea Posta nazo huwaka njano wakati inatakiwa kuwa kijani na wakati mwingine haieleweki na dereva akipita basi hujikuta mikononi mwa polisi ambao hujificha chini ya mti.

Kwa jumla, taa zote nilizozitaja ni maumivu kwa madereva na imekuwa sehemu ya askari kukamata madereva kwa makosa ya usalama barabarani kwamba wamepita kwenye taa nyekundu. Hali hiyo ni maumivu ya kutozwa faini kwa makosa ambayo kimsingi hayapo.

> **"Askari wanachofanya katika eneo la Namanga ni kusimamisha magari yote ya mwisho kwenye kila kundi lililopita na utakuta ni magari matatu au mawili na wote wanaambiwa wanakabiliwa na kosa la kupita kwenye taa nyekundu. Ukibisha wanatishia kukupandisha mahakamani, ikifika mahali kukawa na taa zinazohesabu dakika ni rahisi dereva kujikadiria.**

Kutokana na taa hizi kuwa katika hali hiyo kuna uwezekano mkubwa wa ajali kutokea kwa kuwa dereva ataona taa imemruhusu kumbe kiuhalisia haiko hivyo na wakati mwingine magari kukutana eneo moja.

Lakini kubwa ni ubishani ambao hujitokeza baina ya askari ambao wakati mwingine wanajua wazi matatizo ya taa hizo na kumtaka dereva kutumia taa zingine za mbele yake wakati huo akitaka kwenda kulia.

Askari wanachofanya katika eneo la Namanga ni kusimamisha magari yote ya mwisho kwenye kila kundi lililopita na utakuta ni magari matatu au mawili na wote wanaambiwa wanakabiliwa na kosa la kupita kwenye taa nyekundu. Ukibisha wanatishia kukupandisha mahakamani, ikifika mahali kukawa na taa zinazohesabu dakika ni rahisi dereva kujikadiria.

Kinachozua maswali na wasiwasi ni kuwa askari hao wanajua taa hizo haziko sawa, hivyo kilichotarajiwa ni kuhakikisha marekebisho yanafanyika ili madereva wapite kwa kuzingatia sheria.


Ni vyema Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) wakafanya ukaguzi wa kina wa taa hizo ili kujiridhisha kama zinafanya kazi inavyotakiwa. Kama zinahitaji kuondolewa, kurekebishwa au kusafishwa ikafanyika hivyo mapema au kuzibadilisha na kuweka mpya zinazoruhusu magari kwa dakika jambo ambalo litaondoa uwezekano wa upande mmoja kuruhusiwa sana huku mwingine ukisota.

Taa hizi ambazo baadhi zinafanya kazi unakuta zimefifia kiasi ambacho wakati mwingine dereva anaweza asione vizuri kuwa ameruhusiwa, kazuiwa au anatakiwa kujiandaa kuondoka.

Badala ya taa sasa kutumika kama fimbo kwa madereva wengi ni muhimu Polisi wakawajulisha TANROAD kuhusu ubovu wa taa hizo ili zirekebishwe na kuondoa lawama za kutoza faini umiza.


Pia ni muhimu sana kama wanaona taa hizo zimepitwa na wakati basi ziwekwe taa mpya zenye kuhesabu dakika kama maeneo mengine,ili kuhakikisha dereva anaona dakika na kama akipita basi atakuwa amefanya kusudi.

***Mungu ibariki Tanzania.***









Novemba 27 mwaka huu Phinias Matunda au 'Phinmat Investments' na Christina Magoma, walifunga ndoa katika Kanisa la Mtakatifu Ambros Itibuka, mjini Mpanda mkoani Katavi na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Mpanda. Tunawatakia maisha mema ya ndoa.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# 2021 MWAKA WA VITENGE

MWAKA 2021 umebaki siku chache kumalizika, lakini jambo la kukumbukwa ni jinsi tasnia ya mavazi ilitawaliwa na mitindo mingi ya mavazi.

Mitindo ya kiafrika ni sehemu ya maisha ya wanawake katika kipindi chote cha mwaka, kuna walioshona magauni ya kitamaduni na yale ya kisasa, kila mtu amejimwaga na kile anachokipenda.

Wabunifu wa mitindo wamekuwa na kazi kubwa ya kubuni aina tofauti za nguo ambazo zimewaingizia pesa nyingi.

Mavazi ambayo yalibamba zaidi mwaka huu ni magauni ya vitenge, khanga na vitambaa vingine kama hariri na polista.

Hakika ni kwamba mavazi yaliyoshonwa kwa gharama nafuu yasiyo ya bei kali (simple) yamekuja kwenye mahali pake, lakini ni pamoja na wabunifu nguli na kuliteka soko.

Tuna orodha ya mitindo ya kisasa ya Kiafrika wameifurahia hasa vitenge ambavyo imekuwa chaguo la wengi, lakini pia kuna orodha ya mitindo iliyotawala mwaka 2020.

UREMBO

Na Mary Geofrey



KARABATI NGOZI

# Tango, nyanya, asali vinatosha kukupa furaha

KATIKA shughuli za kila siku suala la kuathirika miili yetu kwa mionzi ya jua limekuwa jambo la kawaida.

Mionzi hii sio tu huifikia ngozi zetu lakini pia huweza kusababisha mabadiliko fulani ambayo hupelekea ionekane imefifia au nyeusi zaidi.

Mfano mzuri mtu akitembea juani kwa muda mrefu utaona rangi ya paji la uso iko tofauti na sehemu nyingine za uso au kwa wale wenzetu wanaovaa nguo zinazoacha wazi maeneo ya kifua au mgongo utagundua rangi za maeneo hayo iko tofauti na sehemu zingine za mwili.

Hali hii inajulikana kitaalamu kama 'suntanning' na hutokea pale ngozi inapozalisha zaidi chembe hai zinazofanya kuwa na rangi nyeusi, ikijaribu kujilinda dhidi ya uharibifu unaoweza kusababishwa na mionzi ya jua.

Leo nimekuandalia njia za asili na rahisi ambazo unaweza kuzitumia ili kusaidia kuondoa utofauti wa rangi ya ngozi unaoletwa na mionzi ya jua.

**NYANYA NA ASALI**

Nyanya kubwa moja na asali (kijiko kikubwa).

Kuna njia mbili unazoweza kutumia kuandaa, unatakiwa kuchukua nyanya, ikate katikati na uchovye asali upande huo ulioukata kisha anza kupaka sehemu husika.

Chukua nyanya uisage na kisha changanya asali na uanze kupaka. Subiri kwa dakika 15 hadi 20, baada ya hapo nawa maji halafu jikaushe kwa kitambaa safi.

Fanya hivi kila siku kupata matokeo yanayo ridhisha.

Tango na Asali

Chukua tango moja na asali kijiko kimoja cha chai,kisha saga na mchanganyiko wake paka sehemu iliyoathiriwa.

Subiri kwa dakika 10 hadi 15 kisha nawa maji. Tumia njia hii mara moja au mbili kila siku.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

PUNGUZA UZITO

# Kwa juisi ya tango

JUISI ya tango itakusaidia kuyeyusha mafuta mengi kwa kipindi hiki unacho jaribu kupunguza uzito.

Unatakiwa kunywa ndani ya siku saba mfululizo ili kupata matokeo mazuri.

Juisi ya tango inasaidia kwa wenye mwili na uzito mkubwa ambao mara nyingi wanashindwa kufanya mazoezi.

**MAHITAJI**

Tango moja kubwa, limao kubwa moja, Tangawizi kipande kimoja, Aloe Vera na maji glasi moja.

**NAMNA YA KUANDAA**

Osha matunda yako na kisha anza katakata Aloe Vera vipande vya saizi na weka kwenye bakuli safi.

Katakata tango bila kulimenya maganda yake na tangawizi pia kata limao na ulikamulie huko kwenye hayo matunda mengine.

Baada ya kukamua limao weka na nyama zake na baada ya kuandaa matunda yote yaweke kwenye brenda pamoja na maji glasi moja.

Saga mchanganyiko wako hadi iwe laini na baada ya hapo juisi yako itakuwa tayari kwa kunyweka.

Kwa kipindi hiki cha kupunguza uzito usichuje juisi kunywa kama ilivyo.

Tumia juisi hii mda wa kulala tu, mara moja kwa siku.



# MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Jifunze namna ya kusafisha sofa

WASWAHILI husema umaridadi huficha umaskini. Hii ni sentesi nzuri kwa kutamkwa lakini pia inatafakarisha.

Katika nyumba, leo tunatazama njia mbalimbali za usafi wa sofa kwenye nyumba.

Kama ilivyo katika usafi mwingine kwenye nyumba pia usafi wa sofa ni muhimu kwa sababu zinakaa kwenye maeneo muhimu ndani ya nyumba. Zisipofanyiwa usafi ipasavyo, huharibika mvuto wake kabisa.

Baadhi yetu huenda tunashindwa kuzifanyia usafi sofa zetu kwa sababu ya kutokufahamu namna ya kuzifanya ziwe nadhifu.

Pia tuko ambao tumekuwa tukifanya usafi wa kawaida siku zote kwa kuzifuta vumbi tu jambo ambalo wakati mwingine haisaidii kung'arisha.

Baadhi ya sofa hutokana na muundo wa malighafi zake, zikifutwa kawaida au kwa kutumia maji matokeo yake huwa si mazuri kwa kuwa badala ya kung'ara huanza kuchafuka na kuchakaa zaidi.

Na ikifikia katika hali hiyo, matokeo yake hata pale unapopata njia sahihi ya kusafisha, huwa hazirudii katika mng`ao wake asili kwa sababu hulazimika kutumia nguvu kubwa na kusugua zaidi jambo ambalo husababisha kupausha rangi au kuondoa mng'aro kabisa.

Kwa wale wanaomiliki sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi ya kusafishia badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu mzuri hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Yako maji maalum au 'spray' inayotumika kusafishia sofa, hivyo ni vema ukaitafuta hiyo kwa sababu inapatikana kwa wingi.

Lakini baada ya kuipata hakikisha sofa zako zimepanguswa na kutolewa vumbi yote iliyokuwa imeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalumu cha kupuliza vumbi au kwa kutumia kitambaa kisafi.

Baada ya kuhakikisha umesafisha kila kona, ndipo unatakiwa kuanza kuipulizia.

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalumu za maji ya kusafishia sofa, unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi hasa kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa naamini moja inaweza kutosha labda uchafu wake uwe wa kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kuhakikisha unaipulizia katika sehemu ndogo ili wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi na unatakiwa kufanya hivyo mpaka umalize.


Baada ya kumaliza kazi hiyo katika maeneo yote unaweza kuliacha likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo mazuri, kwa sababu mng`ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi.

Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa lako hauhitaji gharama kubwa sana endapo utafanya mwenyewe, isipokuwa uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako.

Na pia kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa lako mara kwa mara ndivyo hivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hutatumia spray nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.



## Dondoo za kukifanya chumba kieleze hisia zako kwa mpenzi wako



CHUMBA chako kinakuwa alama nzuri ya kumfanya mtu unayempenda afahamu nini hisia zako pale anapokutembelea kwa mara ya kwanza.

Kutokana na mpangilio wa mapambo ndani ya chumba chako, ni neno tosha kumueleza mpenzi wako kwamba nini unahitaji na kipi unahisi katika moyo wako.

Kulingana na umuhimu wake, hizi ni baadhi ya dondoo ambazo unaweza kufanya kwa ajili ya kukifanya chumba chako kiongee kuhusu hisia zako.


1: Kitanda kipambe kwa kuweka shuka za rangi nyekundu ambazo katikati kuna alama kubwa ya moyo, tandika vizuri ili anapoingia jicho lake ligongane na mandhari ya kitanda.

2: Kama una maua ya waridi unatakiwa kutupia kitandani na sehemu muhimu kama juu ya meza ya kahawa, chini ya kapetii na kwenye sofa dogo ili kutoa harufu maridhawa.

3: Meza ya chumbani inapambwa na mishumaa yenye rangi nyekundu na meupe na kufanya mwanga chumbani kuwa hafifu na usiochosha macho.

4: Weka maua wa zaiada katika meza ndogo za pembeni na kisha weka mishumaa ili kuongeza mandhari ya upendo chumbani.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JAMANI MNATUJAZIA VITANDA! KWANI KUMETOKEA NINI KILA ANAYEKUJA PRESHA IKO JUU AU IKO CHINI?
UPO DUNIANI AU MBINGUNI?
JUKWAANI
INAMAANA HUJUI MTANANGE WA 'WATANI WA JADI' ROHO ZINAKUWAGA 'ZIMESIMAMA WIMA!"
WAGONJWA HOI HOI
HOSPITOL
WANANDOA MKIWA WATANI WA JADI, ' RAHA TUPU!'
KWAKWELI RAHA TUPU! LAKINI UWE UTANI WA MPIRA SIO WAKUNIOLEA MKE MWENZA
UKIOA TU! NAKULIPIZIA NAOLEWA NA MJUMBE
HA HA HA HAAAAA! NILIYOYAONA NITAKUWA NACHEKA MWENYEWE KA' CHIZI KAOZESHWA MKE!
'KAMA NI KWELI MBONA SISIKII LADHA! AU NAOTA???
UTAOTA HADI UTAOTA TENA!
HESHIMU MAKUBALIANO... TUMEPINGA MATOKEO HAYA YA MECHI, UTALALA CHINI HATUKUTANI MIE SITA!
ISHIA HAPO HAPO! UNADHANI WAKISIKIA WALIOTUFUNGISHA NDOA WATATUONAJE? LALA PEKE YAKO UFAIDI!
UKIUMWA 'MJOJO' SITOKI NJE USINIAMSHE'
MAJIRANI NAWASALIMU 'KIPUTE SIO UHASAMA' YALIYOPITA SI NDWELE TUSIKUNJIANE SURA 'TUTAZEEKA HARAKA'
MBONA UNAWEWE-SEKA KAMA MWANGA KANASA KWENYE NYUMBA YA MCHUNGAJI?
ANAJIKOMBA TUMUONEE HURUMA KWA ALICHOKUTANA NACHO!
MSIMBAZI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MBOGA DAGAA, NYAMA HAMU

HABARI KIMATAIFA

# Uganda, DRC zadai kuwaangamiza ADF

**BENI,** DRC

VIKOSI vya jeshi la Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo vimesema kuwa kambi nne za waasi wa Allied Democratic Forces (ADF) ziliharibiwa wakati wa mashambulizi ya angani yaliyotekelezwa Novemba 30, mwaka huu.

Taarifa kutoka kwa vikosi vya serikali zote mbili zilisema kuwa wanamgambo 34 wa ADF walikamatwa na raia 31 wa Congo ambao walikuwa wakishikiliwa mateka wameachiliwa.

Majeshi hayo mawili sasa yameanza kufungua barabara katika maeneo ya karibu na Beni, ambako waasi wanaaminika walikuwa wakiishi.

Oparesheni za ardhini zilisitishwa takriban wiki moja iliyopita, kutokana na ubovu wa barabara.

Jeshi la Uganda liliingia Mashariki mwa Congo kwa mwaliko wa serikali ya DRC, kwa lengo la kuwatimua waasi wa kundi la ADF, ambao wanafungamana na mtandao wa Islamic State na wanahusishwa na mfululizo wa mashambulizi ya mabomu ndani ya Uganda.

Kundi la Islamic State lilidai kuhusika na mashambulizi matatu, yakiwemo milipuko miwili ya mabomu katikati mwa jiji la Kampala Novemba 16.

Serikali ya Congo ilisema kuwa imealika wanajeshi wa majirani zake nchini humo kutokana na ADF kuwa mojawapo ya makundi mengi yenye silaha yanayofanya uharibifu mashariki mwa nchi hiyo.

Kundi la ADF, lililofurushwa kutoka Uganda mwanzoni mwa miaka ya 2000, limekuwa likishambulia na kupora watu, kuua na kuwasajili watoto kwa nguvu kupigana.

Wanasiasa wa upinzani na baadhi ya wachambuzi wamepinga vikali kuingia kwa wanajeshi hao katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Msimamo huo unatokana na utumiaji wa vikosi uliofanywa bila kushauriana au kupata kibali kutoka kwa bunge, kama katiba inavyotaka.

**BBC**



Wafanyakazi wa uokoaji wakiangalia mabaki ya ndege ya Helikopta aina ya Mi-17 yakiwaka moto baada ya muda mfupi kuanguka eneo la Tamil Hindu nchini India juzi. Watu 14 wanahofiwa kufa akiwemo ofisa wa ngazi ya juu wa jeshi la nchi hiyo. **PICHA: EPA-EFE**

# Mataifa ya G7 yaionya Urusi

**LIVERPOOL,** UINGEREZA

MAWAZIRI wa mambo ya kigeni na maendeleo kutoka mataifa tajiri duniani (G7) wameapa kuichukulia hatua kali Urusi baada ya kuishutumu kuzidisha harakati za kijeshi katika mpaka wake na Ukraine. Katika mkutano huo ulioanza jana mjini Liverpool nchini Uingereza, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Liz Truss, aliapa kwamba ulimwengu wa Magharibi na washirika wake utachukuwa msimamo mkali dhidi ya wachokozi wanaosaka kuuhujumu uhuru.

"Mwishoni mwa wiki hii, mataifa makubwa ya kidemokrasia ulimwenguni yatachukuwa msimamo dhidi ya wachokozi ambao wanataka kuuhujumu uhuru na kutuma ujumbe wa wazi kwamba tuko pamoja," alisema Truss.

Aliongeza kwa kutaka mataifa ya G7 kuongeza mashirikiano kwenye maeneo ya biashara, uwekezaji, teknolojia na usalama ili kuulinda na kuupeleka mbele uhuru na demokrasia duniani kote. Mkutano huo wa siku mbili ni wa mwisho wa moja kwa moja wakati Uingereza ikiwa Mwenyekiti na unafanyika wakati dunia ikikumbwa na mitafaruku kadhaa.

Hatua ya Urusi kuongeza wanajeshi kwenye mpaka wake na Ukraine ndiyo ajenda kuu ya mkutano huo, sambamba na kukabiliana na vitisho vya China, kuzuwia mpango wa nyuklia wa Iran pamoja na mzozo wa Myanmar ambako jeshi limechukuwa madaraka tangu Februari Mosi mwaka huu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani,Antony Blinken aliwasili tangu Ijumaa kwa ajili ya mazungumzo ya awali na mwenzake wa Uingereza, Liz Truss, na pia waziri mpya wa mambo ya kigeni wa Ujerumani, Annalena Baerbock.

**DW**

## China, Myanmar zawekewa vikwazo

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imeweka vikwazo dhidi ya watu binafsi na taasisi kadhaa zinazohusiana na nchi za China, Myanmar na Korea Kaskazini kwa sababu ya kukiuka haki za binadamu. Kampuni ya China ya teknolojia ya akili ya bandia "Sense Time" pàia imewekewa vikwazo na Marekani.

Nchi ya Korea kusini haijaepuka vikwazo hivyo, baada ya mapema jana kuongezwa katika orodha ya vikwazo.

Hata hivyo, Canada na Uingereza pia zimejiunga na nchi hiyo katika kuitenga Myanmar na kuweka vikwazo kwa kukiuka haki za binadamu.

Katika hatua nyingine, China imejibu kwa kuishutumu Marekani kwa kuweka vikwazo hivyo na ilisema kuwa hatua hiyo ni ya kujiingiza katika mambo ya ndani ya nchi hiyo na kwamba Marekani inakiuka taratibu za msingi wa uhusiano wa kimataifa. Marekani na nchi kadhaa za Magharibi zinaishutumu China kwa kukiuka haki za jamii ya Waislamu ya Uighur, wapatao milioni moja kwenye jimbo la Xinjiang.

**DW**

## UN yataka kurejeshwa imani Sudan

**NEWYORK,** MAREKANI

MJUMBE wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia masuala ya Sudan, amewataka wanajeshi wa nchi hiyo kurejesha imani kwa wapinzani na vijana wa nchi hiyo wanaohisi kusalitiwa baada ya kufanyika mapinduzi ya kijeshi.

Volker Perthes, ameliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa ufumbuzi utapatikana ikiwa hatua za haraka za kuleta uhuru zitachukuliwa.

Alisema hali hiyo itajizatiti kama juhudi za kurejea kwenye njia ya kuelekea kwenye demokrasia nchini Sudan itafanyika. Kutokana na shinikizo la kimataifa, Waziri Mkuu Abdallah Hamdok, alirejeshwa madarakani mwezi uliopita baada ya serikali yake kuangushwa na wanajeshi Oktoba mwaka huu. Perthes pia alielezea wasiwasi wake juu ya kuibuka tena kwa migogoro baina ya jamii na vitendo vya ujambazi kwenye maeneo ya Darfur, Blue Nile na Kordofans.

Umoja wa Mataifa umepokea ripoti za ongezeko la mauaji ya raia, uharibifu wa mali na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana.

**DW**

## MAKALA

# MIAKA 60 YA UHURU WA TANGANYIKA TUKO WAPI?



Na Magabilo Masambu

"Nchi changa ni sawa na nyumba mpya. Unapojenga nyumba mpya unaifurahia lakini unapotokea mtikisiko utawaonyesheni sehemu mbovu za nyumba ile."

KILA ifikapo Desemba 9 kila mwaka, Tanzania tumekuwa na maadhimisho ya Uhuru wa Tanganyika. Siku hii ni muhimu katika kuhakikisha historia hii haifi vizazi na vizazi.

Sherehe hizo zimekuwa zikitumika kuonyesha mambo mbalimbali zikiwamo shughuli za kijeshi ikiwa ni sehemu ya kuonyesha uimara wa ulinzi wa nchi yetu. Silaha mbalimbali za kivita zimekuwa zikipitishwa mbele ya halaiki na mbele ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sambamba na gwaride maalumu linalojumuisha majeshi yetu ya ulinzi na usalama. Yote hiyo ni kupamba sherehe hizo.

Jambo mojawapo tunaloweza kujivuna kwa kiasi kama sehemu ya mafanikio ya Uhuru ni umoja wetu. Baadhi ya watanzania hudhani kwamba Tanzania ilijikuta tu wamoja. Pamoja na kwamba tuko zaidi ya makabila 120, tunazo dini mbalimbali na bado tumedumu kama ndugu kwa muda wa miaka 60 sasa.

Kusema kweli tukiachana na mbwembwe za baadhi ya wanasiasa, naweza kukiri kabisa kwa dhati kuwa sisi bado ni wamoja. Wananchi wa kawaida bado tunapopata matatizo, tunasaidiana kama ndugu. Kwa upande mmoja, hayo yanaweza kuwa maendeleo ya kijami. Licha ya kwamba yanaweza kuwa hayajakamilika, angalau tunaweza kujisifu.

Machi 13, 1995 kuelekea uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi uliofanyika Oktoba, mwaka huo, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye ni muasisi wa taifa hili, akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari katika hoteli ya Kilimanjaro.

Katika mkutano huo, alisema: "Nchi changa ni sawa na nyumba mpya. Unapojenga nyumba mpya unaifurahia lakini unapotokea mtikisiko utawaonyesheni sehemu mbovu za nyumba ile."

Akasema anaziona nyufa katika paa, kuta lakini pia katika msingi. Akataja nyufa tano ambazo ni Muungano, kupuuza na kutojali Katiba ya nchi, kuendesha mambo bila kujali sheria, rushwa na tano akasema ukabila na udini.

Leo ni miaka 60 ya Uhuru tuko wapi? Haya ni maswali tunayopaswa kujiuliza kama Watanzania. Sitaki kuamini kwamba tumeshakuwa na hali mbaya katika maeneo yote hayo, nafikiri kama kuna maeneo yameanza kujitokeza lazima hatua za makusudi zichukuliwe kurekebisha nyufa hizo.

Katika eneo la maendeleo ya vitu na watu, pengine tunaweza kujivuna kwamba tukilinganisha maendeleo tuliyo nayo leo miaka 60 baada ya Uhuru na yale ya miaka michache baada au kabla, kuna jambo limefanyika katika elimu, afya na maeneo mengine japo hatuwezi kujivuna sana kulingana na muda tuliojitawala. Kwa hiyo juhudi za mwananchi mmoja mmoja pamoja na serikali zinatakiwa kuongezeka kwa kasi zaidi ili kujiletea maendeleo yaliyokusudiwa badala ya kutegemea kina mjomba.

Eneo la sheria pia linapaswa kutazamwa upya na pengine kufanyiwa mabadiliko kwa sababu kama tutakuwa tumejitawala lakini tukaendelea kutumia sheria za mkoloni maana halisi ya kuwa huru inakosa uhalali.

Tulipambana kujikomboa dhidi ya ukandamizaji wa wakoloni ambao walitumia sheria kutukandamiza. Maana yake kama sheria walizotumia bado tunazo kwenye mifumo yetu ya kiutawala, basi tutakachokuwa tumebadili ni sura za watu.

Miaka 60 ni mingi sana, hata zisingekuwa sheria za kikoloni mambo mengi yamebadilika pia, hivyo yanahitaji mabadiliko ya kisheria. Si dhambi kufanya marekebisho ya Katiba ya nchi ili iendane na matakwa ya Watanzania wa miaka 60 baada ya Uhuru na kuwafaa wengine miaka mingi zaidi.

Baada ya hapo huko mbele watakuwa wanabadili kulingana na mahitaji ya kimaendeleo. Nakubali kwamba si yote ni mbovu lakini kama tunaona kuna matundu kwa pamoja kwa umoja wetu, tunaweza kukubaliana kubadili baadhi ya maeneo kwa maslahi ya taifa na si kwa ajili ya kikundi au mtu binafsi.

Kwetu wananchi, katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru ni muhimu pia kubadili dhana ya maendeleo ili iwe kazi zaidi kuliko kudhani fedha zitamaliza shida zetu. Fedha ni matokeo ya kazi na hili halina budi kufanywa zaidi na viongozi wetu. Tuhamasishe watu wazalishe zaidi mashambani ili wawe na chakula cha kutosha. Ziada watauza na kupata fedha ili inapofika vipindi vya uchaguzi, wananchi wasiwachague viongozi kwa sababu ya njaa kwa kuhongwa vitu visivyowasaidia.

Bahati mbaya tuliyo nayo ni matatizo ya umasikini wa wananchi kuendelea kutumika kama mtaji wa kisiasa. Ni muhimu sherehe hizi za siku ya uhuru pamoja na kujikumbusha mambo mengi yanayohusu siku yenyewe, zaidi zitukumbushe shida za watu wetu kwa miaka 60 ni kwa namna gani zitaendelea kutatuliwa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Photo Album', gauni, picha vyavunja ndoa



Na Adam Fungamwango

"Photo albamu inaleta maneno, katikati ya mji wa Mwanza. Kisa ni picha iliyopigwa zamani, katikati ya Dar es Salaam. Sheri Zinduna nakupa pole Zinduna."

WAMENIAMBIA mambo yako mama eee, wamenieleza matatizo ya mume wako eee, ya kisa cha wewe sheri Zinduna, kufika kupewa talaka."

Ni mwanzo wa wimbo uliotungwa na gwiji la muziki Tanzania, Zahir Ally Zorro, akiwa na bendi ya Kimulimuli Jazz iliyokuwa ikimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na maskani yake yalikuwa Mafinga mkoani Iringa. Mwanamuziki huyu ndiye baba wa mwanamuziki Banana Zorro.

Ni wimbo huo unaoitwa 'Kisa cha Photo Album' una kisa kimoja cha ajabu na kusikitisha sana.

Nimeamua kuja na mada hii leo ili tuangalie wanamuziki wa zamani walivyokuwa na uwezo wa kuchukua visa vya kweli kabisa na kuviweka kwenye muziki, vikafundisha, kuelimisha, kufurahisha na kufikirisha watu.

Hiki ni kisa cha ukweli kabisa kilichotokea kwenye miaka ya 1980. Ni kisa cha picha iliyopigwa zamani katikati ya jiji la Dar es Salaam, lakini ikaenda kuvunja ndoa miaka mingi baadaye jijini Mwanza. Hebu tuendelee na mashairi ya wimbo huu.

*"Photo albamu inaleta maneno, katikati ya mji wa Mwanza. Kisa ni picha iliyopigwa zamani, katikati ya Dar es Salaam. Sheri Zinduna nakupa pole Zinduna. Matatizo yanayokukuta. Mkasa nyumbani kwako, ndoa imevunjika, kisa ni picha ya zamani ooo. Afadhali kama mimi ningewahi kufika Mwanza, lakini tangu mimi nimezaliwa, sijafika Mwanza ooo. vitongoji vya Nyamanoro, Kirumba na Mtaa wa Sukuma, nimeelezwa na wenyeji ooo."* Hapa ndipo wimbo huo ulipokamilika.

Maudhui ya wimbo huu, ni kwamba huyu dada Zinduna aliolewa na jamaa jijini Mwanza. Lakini kabla ya kuolewa alikuwa na mpenzi wake. Waliwahi kupiga picha katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Mwanadada huyo inaonekana alihifadhi picha hiyo sehemu ambayo anaijua yeye hata baada ya kuachana na mpenzi wake huyo na kupata mchumba ambaye alikuja kumuoa, akawa mumewe. Baada ya kuolewa, makazi ya Zinduna na mumewe yakahamia jijini Mwanza kutoka Dar es Salaam.

Kilichotokea baada ya miaka michache, mume wa Zinduna aliifuma picha ya mkewe aliyopiga na mpenzi wake katikati ya jiji la Dar es Salaam. Sijui ilikuwaje, lakini aliifuma picha hiyo iliyofichwa vizuri kwenye 'photo albamu'.

Mume alichanganyikiwa na kwa bahati mbaya sana ni kwamba gauni alilovaa Zinduna lilifanana sana na lile alilomnunulia siku chache zilizopita kabla ya kitimtimu hicho.

Mume akiangalia anaona ni kama picha ya zamani ambayo haikupigwa Mwanza, lakini hayo yote yanamezwa na gauni hilo alilomnunulia karibuni. Akawa anajiuliza kama ni picha ya zamani, mbona gauni hili ndiyo hilo alilomnunulia majuzi.

Kwa hiyo akadhani kabisa kuwa picha hiyo haikupigwa siku nyingi. Kwa hiyo akaona kabisa kuwa kumbe mkewe anamsaliti.

Pamoja na Zinduna kujitetea kwa anavyojua kuwa picha hiyo ni ya mpenzi wake wa zamani, miaka zaidi ya 10 iliyopita kabla hata ya kukutana na yeye, tena ilipigwa Dar es Salaam, mume hakukubali. Kilichofuata ni talaka. Zinduna alilia na kusononeka. Akarejea kwao Dar es Salaam.

Mpenzi wa zamani ambaye alipiga naye hiyo picha akasikia habari hizo. Alisikitika sana na hakujua afanye nini ili amsaidie kwani naye alikuwa ameshaoa. Basi akabaki na yeye analalamika na kumpa pole mpenzi wake wa zamani Zinduna.

Anayesikika anaimba kwenye wimbo huo kwa jinsi ulivyopangiliwa, ndiye mpenzi wa zamani wa Zinduna. Anamwambia wameniambia mambo yake na matatizo yake na kisa cha mpenzi wake wa zamani Zinduna kufika kupewa talaka, kisa ni 'photo albamu' iliyokuwa na picha waliyopiga zamani katikati ya Dar es Salaam, ikaleta maneno Mwanza.

"Alipaswa baba watoto ajue, sijawahi kufika Mwanza, toka mimi nizaliwe, sijafika Mwanza." Jamaa anamfariji mpenzi wake wa zamani kuwa mumewe alipaswa ajue kuwa yeye hajawahi kufika Mwanza tangu azaliwe, hivyo hiyo picha siyo ya hivi karibuni bali ya zamani kabla hajaolewa. Kama angewahi kufika Mwanza, basi angekuwa na wasiwasi kuwa amepiga picha na mkewe, lakini vitongoji vyote anavisikia kwa watu.

Wimbo huu unaikumbusha jamii kuwa kuna wakati watu wanafanya uamuzi mgumu kwa vitu ambavyo hawajavifanyia utafiti wa kutosha au kufanya upepelezi, bali ni hasira na mihemko.

Ni kwamba inafaa kwanza kabla ya kuamua jambo lolote hasa lenye mustakabali wa maisha yetu, ni lazima tujiridhishe kwanza. Zinduna amepewa talaka kwa kosa ambalo hajalifanya. Mumewe kama alikuja kujua hilo baadaye anaweza kumshawishi mkewe warudiane? Na kama akikataa kuna kosa?

**Meseji namba: 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-8

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

EDDY alifurahi kwani tayari kazi yake ilikuwa imeanza vizuri. Sio kwamba hakujua kama Mwahija alikwenda kutoa ushahidi mahakamani. Alichotaka ni kuwa na uhakika na ushahidi kuwa ni kweli Tina alikwenda kununua dawa ambazo zilimuua Chilambo. Hii kwake ingeweza kumsaidia anapoelekea kwenye upelelezi wake. Anatakiwa awe na uhakika na kila kitu ili kupata vielelezo sahihi. Na wakati huo alikuwa anarekodi kupitia kifaa chake cha kunasa sauti kama vinavyotumiwa na waandishi wa habari kuhoji watu. Lakini hiki ni kifaa kidogo ambacho huwa hakionyeshi. Kinakaa mfukoni tu.

Mwahija yeye alionekana kupata rafiki mcheshi. Mwenye maneno matamu ya kuvutia. Mtu ambaye hachoshi kumsikiliza. Pamoja na kwamba alikuja kuulizia habari za mpwa wake na kumpa ukweli, hakuonekana kusononeka, wala kumkasirikia. Ndiyo kwanza anamuomba ampeleke akaione nyumba ya marehemu Chilambo ambayo kwa sasa inaishi familia yake.

Mwanzoni alihofu kuwa inawezekana ni njama ya mtu yule ili alipize kisasi cha mpwa wake. Lakini moyo wake ulikataa. Ilitokea tu ghafla akaanza kumuamini mtu yule. Hakujua kwa nini.

"Da' Fatuma, natoka kidogo, nampeleka mgeni wangu hapo mbele, narudi sasa hivi." Ilikuwa ni sauti ya Mwahija akimuaga mwenzake aliyekuwa naye kwenye duka hilo.

Fatuma alitabasamu. Kama kuna kitu alitaka kuongea, lakini maneno hayakutoka. Ni kwa sababu alisikia vicheko ndani ofisini.

Mwahija alijua nini ambacho Fatuma anafikiria baada ya kuona anaangaliwa na tabasamu lililoishia na kicheko cha chini chini.

"Yatakushinda." Mwahija alimsindikiza kwa sauti ya chini.

"Ahsante sana bibie, nakuomba radhi kidogo, namchukua mwenzako huyu, namrudisha punde tu, hatuendi mbali." Eddy alimtaka radhi Fatuma.

"Hata ukimrudisha kesho sawa tu, kwa jinsi alivyokuwa anakujibu mwanzo. Nashangaa sijui umemwambia nini huko nasikia vicheko tu, wakati mwanzo alikuwa mkali kama pilipili." Fatuma alimjibu Eddy alikuwa anampiga kijembe Mwahija.

"Bibi ee unatuchelewesha." Akajibu Mwahija huku akifungua mlango na kuruhusu mgeni wake atoke na yeye akafuatia.

*******************************

Yalikuwa ni matembezi yaliyofurahiwa na wote wawili. Walitembea taratibu. Baadhi ya watu waliwatazama. Baadhi walimfahamu Mwahija kwa sababu huwa anawauzia dawa, lakini hawakumfahamu Eddy.

Wengine walijua ni mpenzi wake. Wengine wakadhani ni mumewe. "Hii ndiyo nyumba ya marehemu Hafidh Chilambo." Mwahija alimuonyesha Eddy jumba moja la fahari lililokuwa na geti jeusi. Pembeni kulikuwa na kikaratasi chenye maandishi kuwa wanauza barafu, maji baridi na ice cream.

"Okay, kumbe mpwa wangu alikuwa anafanya kazi hapa."

"Ndiyo." Eddy kama ilivyo kawaida yake, alilitazama eneo lile kipelelezi. Alipochungulia ndani aliona magari mawili yakiwa yamepaki. Moja jeupe na lingine rangi ya bluu. Hakubahatika kunakili namba, lakini kwa ujanja wa hali ya juu, alifanikiwa kupiga picha eneo hilo, lilionyesha taswira yote ya geti, magari pamoja na bustani. Aliona huenda ikamsaidia baadaye.

"Sasa hivi anakaa nani?"

"Mkewe na watoto."

"Hivi sasa inawezekana ana mfanyakazi mwingine wa ndani."

"Mh! hapo sasa sijui, wewe nawe maswali yako, kama polisi vile."

"Unaonaje tukienda kubonyeza kitufe, wafungue mlango tuone."

"Halafu wakifungua."

"Tununue maji baridi na ice cream." Jibu hilo lilifuatia kicheko kutoka kwa Mwahija.

"Unajua wewe una mzaha, yaani sisi wakubwa wazima tununue ice cream na maji baridi kweli?"

"Mimi ninakunywa maji baridi, wewe nakununuliwa ice cream."

"Ndugu yangu tutachekesha tu walionuna na hata wao wanaweza kutushangaa na kuwa na wasiwasi na sisi. Yaani tulivyo tuwe hatuna uwezo wa kununua hata maji ya chupa kweli, tukanunue barafu na ice cream."

Nia ya Eddy haikuwa hivyo. Alichotaka ni kuendelea kuongea na Mwahija ili amzoee. Katika mafunzo yake walishawahi kuambiwa ili mtu akuzoee na asiwe na shaka sana na wewe ni lazima mazungumzo yawe ya kawaida sana, yasiyo magumu ambayo yatamchosha anayesikiliza.

Yalikuwa mazungumzo ya mzaha zaidi ambayo Mwahija kuna wakati alijua ni kweli, lakini kuna wakati anajua ni mzaha.

Walifika kwenye duka moja kubwa, Eddy alimshika mkono Mwahija na kumwambia "Hebu tuangalie hapa dukani kuna nini?" Eddy alinunua mikate mitano mikubwa na kumkabidhi Mwahija.

"Kwa leo hii zawadi yangu kwako."

"Eeh, nashukuru sana kaka."

"Sasa turudi kule kule tulikotoka. Kila mtu anayetuona atajua kuwa tulikuja dukani."

"Mh! kweli mwaya. Maana watasema wale walikwenda huku, halafu wamerudia njiani." Ulikuwa ni mwendo mrefu kidogo, kutoka walipotoka hadi Eddy alipoacha gari lake Nissan Ariya.

Ukawa ni mshangao mwingine kwa Mwahija. Jinsi mgeni huyo alipokuja hakuonekana kama alikuja na gari. Alionekana kama alikuja tu labda na bodaboda au daladala na kushukia alikoshuka. Kama angekuja na gari basi angekuja nalo hadi mlangoni. Ni kwa nini aliliacha gari mbali namna hiyo?

Ni swali ambalo alijiuliza Mwahija, lakini hakulitilia maanani. Halikuwa na maana yoyote kwake.

"Sasa Mwahija, tutaonana. Nashukuru kupata mwenyeji hapa. Nashukuru kwa ukarimu wako, hasa huku mwishoni, japo mwanzo ulikuwa matata kidogo, nitakuja tena. Lakini safari hii ni kwa ajili yako." Alisema huku akitoa noti ya shilingi efu kumi na kumkabidhi "Utafanya nauli."

"Du, nashukuru sana, maana nadaiwa pesa ya mchezo, siku mbili sijalipa." Alijibu Mwahija, lakini sekunde chache baadaye akajiona kama ameropoka tu kwa sababu wala hakuwa na sababu ya maana ya kujibu vile.

Hata hivyo alijiona kama kuna kitu ambacho kilimsukuma kusema maneno yale. Ni kitu ambacho hata mwenyewe hakijui kwa kawaida ni msiri sana. Lakini kwa Eddy anajikuta akiongea baadhi ya maneno ambayo kwa kawaida asingemwambia yeyote yule.

"Ahadi yetu si unaikumbuka?"

"Ipi?"

"Aah, mara hii umesahau?"

"Tumeongea mengi."

"Ya nywele."

"Ahaaa. Nitafumua baada ya siku tatu."

"Basi mimi nitakutumia pesa ya kusukia, kama nilivyokuahidi."

"Nitashukuru."

***************************

"Eeee shoga, na mikate juu."

"Bibi weee yatakushinda, yaani umeshapekua na kuona mikate?"

"Si ulimjibu vibaya kaka wa watu mwanzo wewe, tena sema yule hana hasira, ingekuwa mwingine mngekorofishana, lakini kaenda na wewe taratibu hadi kakunasa." Fatuma alikuwa akimpasha mwenzake.

"Wapi, hajaninasa wala nini?"

"Yaani unanifanya mimi mtoto mdogo, vile vicheko vya ndani ofisini vilikuwa vya kawaida vile. Tofauti ni lile jicho ulilokuwa unamuangalia mwanzo alipokuja hapa na kuuliza maswali."


"Da Fatu, humjui yole, anachekesha. Yaani ni mcheshi, ukikaa naye yule utakuwa unafurahi tu."

"Ndiyo maana naona baada ya kuja yule kaka, umekuwa na furaha sasa. Haya sisi tupo tutayaona."

**ITAENDELEA JUMAPILI**




**"Da' Fatuma, natoka kidogo, nampeleka mgeni wangu hapo mbele, narudi sasa hivi." Ilikuwa ni sauti ya Mwahija akimuaga mwenzake aliyekuwa naye kwenye duka hilo. Fatuma alitabasamu. Kama kuna kitu alitaka kuongea, lakini maneno hayakutoka. Ni kwa sababu alisikia vicheko ndani ofisini.**



# KANYE WEST KUMRITHI VIRGIL UBUNIFU MAVAZI

RAPA maarufu kutoka Marekani, Kanye West anapigiwa chapuo kurithi nafasi ya marehemu Virgil Abloh, ya kuwa mbunifu mkuu wa mavazi ya kiume katika kampuni ya mavazi ya Louis Vuitton.

Kanye na Abloh walikuwa marafiki na walikutana kwa mara ya kwanza na kufanya kazi pamoja mwaka 2009 katika kampuni ya mavazi ya Fendi ya nchini Italia.

Gazeti la The Sun la nchini Uingereza limemtaja Kanye West kama mtu anaeongoza kwa kupigiwa chapuo katika kampuni ya Louis Vuitton kwa ajili ya kuchukua mikoba ya Abloh aliyefariki kwa ugonjwa wa saratani Novemba 28 mwaka huu.

# NED MUSIC

## KUMBE UNAMWOGOPA BELLA



MWANAMUZIKI wa Bongon Fleva, Ned Music, amesema kwake ni jambo la kujifunia kufanya kazi na mkongwe wa muziki nchini Christian Bella.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Ned Music, alikuwa na hofu wakati alipoingia studio kutengeneza wimbo wao wa kwanza akiogopa kumezwa na msanii huyo ambaye ni mahiri katika uimbaji.

"Nakumbuka niliwahi kumwambia prodyuza Aby Dad kuwa akimaliza Bella kuingiza sauti basi kesho nitarudi kuandika upya, walicheka sana lakini kitu kizuri alipenda mistari yangu," amesema Ned Music.

# Smollett utaonja chungu ya uwongo

MWIGIZAJI wa Marekani Jussie Smollett, amekutwa na hatia ya kuidanya polisi alipodai kuwa mwathiriwa wa shambulio la ubaguzi wa rangi, chuki za watu wa mapenzi ya jinsia moja.

Katika kesi wiki hii, Smollett (39), alisimama na kukanusha kwamba aliandaa shambulio la uwongo dhidi yake mwenyewe.

Alipatikana na hatia siku ya Alhamisi ya makosa matano ya kufanya fujo. Kila kosa lina adhabu ya hadi miaka mitatu jela.

Kwa kuzingatia makosa ya Smollett na hatia aliyopatikana nayo, wataalamu wamesema kuna uwezekano wa kutolewa hukumu nyepesi au kuachiwa kwa masharti.

Kesi hiyo ilitokana na kisa cha karibu miaka mitatu iliyopita, wakati nyota huyo wa zamani wa kipindi cha televisheni cha Empire alipowaambia polisi kuwa alikuwa mwathirika wa shambulio.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO KURUDI REAL MADRID
REAL Madrid wanafuatilia hali ya Cristiano Ronaldo katika klabu ya Manchester United. Klabu hiyo ya La Liga inaamini kuwa mkataba wa mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36 unaweza kusitishwa Januari baada ya kuwasili kwa Ralf Rangnick hapo Old Trafford. ***(Football Insider)***

### HAIDARA ATAKIWA MAN
KOCHA wa muda wa Manchester United, Rangnick ameishauri klabu hiyo kumfuatilia kiungo wa kati wa RB Leipzig na Mali, Amadou Haidara mwenye umri wa miaka 23.

### BELLINGHAM, PHILLIPS WAWANIWA
KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18, na kiungo wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26 wanawaniwa Manchester United. ***(ESPN)***

### CHELSEA KUUZA, KUNUNUA
CHELSEA inafikiria uwezekano wa kumnunua beki wa Leicester na Ufaransa wa chini ya umri wa miaka 21, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 20, huku beki wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye miaka 28, na mchezaji wa kimataifa wa Denmark, Andreas Christensen mwenye miaka 25, wakiwa bado hawajasaini mkataba mpya pale Stamford Bridge. ***(Goal)***

### RUDIGER KULIPWA ZAIDI
MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger anatazamiwa kuwa mmoja wa mabeki watakaolipwa fedha nyingi zaidi katika soka iwapo ataamua kuondoka hapo Stamford Bridge, huku klabu kadhaa za Ulaya zikiwa tayari kumuongezea mara nne ya mshahara wake wa sasa. ***(Mail)***

### MARTIAL AGOMBEWA
KLABU za Newcastle United, Barcelona, Arsenal na Paris St-Germain zinaongoza katika kinyang'anyiro cha usajili wa mshambuliaji wa Manchester United Mfaransa Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

### BARCA KUIMARISHWA
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema klabu yake inaelekea katika mwelekeo sahihi na kikosi cha kwanza kitaimarishwa katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Marca)***

### TORRES ANUKIA BARCA
BARCELONA wameongeza dau lao la kumnunua winga wa Hispania na Manchester City, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21, kwa hadi euro miliomi 45 pamoja na malipo mengine ya ziada ya euro milioni 15. (Sport)

### ALVAREZ ATAKIWA
KLABU ya Barcelona pia inamnyatia mshambuliaji wa River Plate na Argentina wa miaka 21, Julian Alvarez, ambaye ana kifungu cha kuondoka cha euro milioni 25. ***(Sportitalia via AS)***

### RAMSEY KUONDOKA
KIUNGO wa kati wa Wales, Aaron Ramsey anataka kuondoka Juventus Januari, huku Everton na Newcastle zikionesha nia ya kutaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Gazzetta dello Sport via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RANGNICK: SITAMSHAWISHI POGBA KUBAKI

**●●●Asema mchezaji akitaka kuondoka hawezi kumzuia, kwani anatakiwa...**

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa muda Ralf Rangnick amesema hatajaribu kumshawishi kiungo, Paul Pogba kubakia Manchester United kama akifanya maamuzi ya kuondoka.

Pogba mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na United kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwa kipindi hicho ya pauni milioni 89 kutoka Juventus mwaka 2016.

Hata hivyo, mshindi huyo wa kombe la Dunia mkataba wake unamalizika wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja na atakuwa huru kuzungumza na klabu nyingine Januari.

"Siwezi kusema kwamba hana thamani ya kumbakiza, lakini wachezaji wanahitaji kutaka kubaki na kucheza kwa klabu," alisema Rangnick.

"Kama mchezaji hataki kuichezea klabu kama Manchester United, hata kwa muda mrefu, sidhani kama inaleta maana kujaribu kumshawishi kubadilisha maamuzi yake.

"Hii ni klabu kubwa, yenye mashabiki wa kuvutia, sidhani kama klabu inatakiwa kujaribu kumshawishi mchezaji kubaki.


"Tunatakiwa kuwa pamoja kama klabu, kujifua vya kutosha na kufanya mazoezi na timu, halafu tutaangalia wapi tumesimama."

Pogba amekuwa nje kwenye kikosi cha United kwa mechi saba zilizopita baada ya kuumia paja kwenye mazoezi akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa ya Ufaransa.

MECHI KALI
HOME AWAY
PARIS ST GERMAIN
1.50 | 4.49 | 5.62
MONACO
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# ARTETA KUTOMUUZA AUBAMEYANG JANUARI



**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta hajajadili wazo lolote la kumuuza nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang katika dirisha la Januari, lakini anatambua kwamba, straika huyo anapitia "magumu."

Aubameyang alitajwa kwenye benchi kwa washikabunduki hao wakati wakifungwa 2-1 na Everton Jumatatu, na aliingia uwanjani dakika za mwisho, akikosa nafasi ya kusawazisha kwenye sekunde za mwisho pale Goodison Park.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye alisaini mkataba mpya pale kwenye dimba la Emirates Septemba mwaka jana, amefunga mabao manne tu na kutoa asisti moja kwenye mechi 14 za Ligi Kuu msimu huu, ikiwa na wastani wa bao moja kila baada ya dakika 259.75.

Uwezo wa Aubameyang kufunga mabao kwa Arsenal umeshuka sana kwa kipindi cha miaka michache iliyopita, ikifananishwa na wastani wa bao moja kila baada ya dakika 105.8 kipindi cha kwanza cha msimu wa 2017-18.

Halafu akafuatiwa na wastani wa bao moja kila dakika 124.14 kwa msimu wote, halafu wastani wa bao moja kila bada ya dakika 142.64 msimu wa 2019-20, na wastani wa bao moja baada ya dakika 233.6 msimu uliopita.

Hata hivyo, kocha wake amepaza sauti ya kupewa sapoti kwa mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, akisema: "Kwa kawaida mchezaji anapokuwa hafungi inaathiri kujiamini kwake."

"Pia inaathiri akili yake na kupunguza uwezo wake dimbani, hivyo ni lazima apewe sapoti kwa namna yoyote ile."

Alipoulizwa kuhusu mahusiano yake na nahodha huyo baada ya kumuacha kwenye mchezo wa Everton, Arteta aliongeza: "Nina mahusiano mazuri na kila mchezaji wangu."

Aubameyang amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Arsenal Januari, na Arteta akasema.

"Kiukweli hatujajadili kitu chochote kuhusu kitu kama hicho," alisema.

# Deschamps akataa kumwondoa Mbappe



**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa timu ya taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps amekanusha madai kwamba amemshauri Kylian Mbappe kuondoka Paris Saint-Germain na Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, mwishoni mwa msimu huu.

Mbappe amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Real Madrid katika misimu ya hivi karibuni wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika kule PSG.

Pia kuna ishara ndogo sana kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuongeza mkataba mpya hapo Parc des Princes.

Katika mahojiano na RMC Sport, Deschamps alisema hajawahi kumshauri Mbappe kuondoka kwenye Ligi ya Ufaransa na kwenda nchi nyingine.

"Huu ni upuuzi kusema kwamba, nilisema (Mbappe) anatakiwa kuondoka Ufaransa," alielezea.

"Kamwe sijawahi kusema hivyo, sio kwake tu hata kwa mtu mwingine yoyote.

"Kylian mwenyewe ndo atachagua wapi anataka kwenda, ni maamuzi yake mwenyewe. Na sio tatizo kama akiamua kubakia jijini Paris."

LIVE IN PLAY

# DTB, IHEFU ZAKARIBIA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya DTB imeendelea kujikita kwenye msimamo wa Ligi ya Championship kwa kuitwanga Mwadui FC mabao 2-0 juzi, na kufikisha jumla ya pointi 27, ikiwa haijapoteza mechi yoyote hadi sasa.

Wakati DTB ikionekana haina mpinzani kwenye ligi hiyo kiasi cha kuwasha indiketa kutinga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, timu iliyoshuka daraja msimu uliomalizika, Ihefu FC, nayo inaonekana kutamani kurejea Ligi Kuu msimu ujao,kwani inashika nafasi ya pili kwenye Championship kwa pointi 20 ilizonazo.

DTB imecheza mechi 11 hadi sasa ikishinda mechi nane, na sare tatu, ikiwa haijapoteza mechi yoyote ile mpaka sasa, huku Ihefu ya Mbarali ikicheza mechi 10, ikishinda sita, ikitoa sare mbili na kupoteza mechi mbili pia.

Wakati timu hizo mbili zikionekana kufukuzana, Kitayosce ya Tabora inakamata nafasi ya tatu ikiwa na pointi 19, ikicheza mechi 10, kushinda sita, sare moja, ikipoteza mechi tatu.

Gwambina FC, ambayo ilishuka daraja msimu uliopita, inashika mkia kwenye ligi hiyo ikiwa na pointi nne tu na haijashinda mechi yoyote ile mpaka sasa.



Vijana wakifanya mazoezi ya kucheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viwanja viwili kufungiwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Zanzibar (ZLB) imesema inaangalia uwezekano wa kutovitumia viwanja viwili vya Ngome na Cairo vinavyochezewa ligi daraja la kwanza kanda ya Unguja kutokana na sababu mbalimbali.

Akizungumza na gazeti hili, Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Sheha Mohamed Ali alisema uwanja wa Ngome eneo lake la kuchezea haliridhishi kutokana na kuwepo kwa mashimo yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Alisema uwanja huo pia umetengeneza mashimo ambayo yanawapa tabu timu pale zinapocheza michezo ya ligi daraja la kwanza inayoendelea.

Aidha alisema kuwa uwanja huo ambao unatumiwa na timu ya Bridge Star kama uwanja wao wa nyumbani, tayari wameshakutana na timu hiyo ambapo wameridhia bodi ya ligi kuwahamisha na kuwapeleka katika uwanja itakao ona unafaa.

Akiuzungumzia uwanja wa Cairo uliopo Kiwengwa unaotumiwa na timu ya African Coast, alisema umekuwa na fujo kubwa pale timu yao inaposhuka dimbani.

Alisema mara kwa mara mashabiki wa timu hiyo wamekuwa na utovu wa nidhamu usiostahamilika hali iliyoifanya bodi ya ligi kuufunga. Hata hivyo, alisema kuwa iwapo watakubaliana mambo kadhaa na uongozi wa timu hiyo pamoja na bodi ya ligi, watawaruhusu kuendelea kuutumia.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 12 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4723 | Dinamo Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.29 | 3.49 | 2.04 |
| 14:15 | 2716 | Twente vs Waalwick | 1.56 | 4.02 | 5.29 |
| 14:30 | 1759 | Torino vs Bologna | 2.27 | 3.25 | 3.20 |
| 15:00 | 2009 | Lille vs Lyon | 2.35 | 3.48 | 2.84 |
| 15:00 | 5727 | Hearts vs Rangers | 5.10 | 4.02 | 1.59 |
| 15:30 | 5276 | Royal Antwerp vs Standard Liege | 1.90 | 3.56 | 3.75 |
| 15:30 | 5889 | Vietnam vs Malaysia | 1.58 | 3.56 | 5.39 |
| 16:00 | 4934 | Villarreal vs Rayo Vallecano | 1.78 | 3.70 | 4.40 |
| 16:15 | 5818 | BSC Young Boys vs FC Sion | 1.23 | 6.33 | 9.89 |
| 16:30 | 3191 | Bloemfontein Celtic vs Golden Arrows | 2.16 | 3.04 | 3.48 |
| 16:30 | 4604 | Groningen vs Feyenoord | 5.50 | 4.22 | 1.51 |
| 16:30 | 5255 | Admira Wacker vs Rapid Vienna | 3.47 | 3.47 | 1.91 |
| 16:30 | 5588 | Vitesse Arnhem vs Heracles Almelo | 1.71 | 3.78 | 4.33 |
| 17:00 | 1113 | Angers vs Clermont Foot | 2.06 | 3.33 | 3.58 |
| 17:00 | 2098 | Leicester vs Newcastle | 1.74 | 4.02 | 4.22 |
| 17:00 | 2446 | Metz vs Lorient | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 17:00 | 2820 | Burnley vs West Ham | 3.50 | 3.55 | 2.03 |
| 17:00 | 3286 | Rennes vs Nice | 1.89 | 3.58 | 3.88 |
| 17:00 | 3348 | Verona vs Atalanta | 3.65 | 3.85 | 1.90 |
| 17:00 | 4113 | Wisla Plock vs Legia Warszawa | 2.84 | 3.13 | 2.33 |
| 17:00 | 5115 | Troyes vs Bordeaux | 2.24 | 3.44 | 3.04 |
| 17:30 | 4376 | Greuther Furth vs Union Berlin | 4.57 | 3.93 | 1.69 |
| 18:00 | 1147 | Dynamo Kiev vs Zorya Lugansk | 1.33 | 4.82 | 7.13 |
| 18:00 | 2939 | Celtic vs Motherwell | 1.15 | 7.10 | 14.79 |
| 18:15 | 2249 | Osasuna vs Barcelona | 3.77 | 3.38 | 2.00 |
| 18:15 | 4713 | PAOK vs Lamia | 1.18 | 6.29 | 14.74 |
| 18:30 | 4865 | Grasshoppers vs FC Luzern | 2.08 | 3.55 | 3.20 |
| 18:45 | 1824 | Ajax vs AZ Alkmaar | 1.22 | 6.49 | 9.44 |
| 19:00 | 4875 | Lokomotiv Moscow vs Ufa | 2.04 | 3.24 | 3.54 |
| 19:00 | 5352 | Kaizer Chiefs vs Sekhukhune United | 2.06 | 3.09 | 3.68 |
| 19:00 | 5675 | Austria Vienna vs LASK Linz | 2.60 | 3.33 | 2.41 |
| 19:00 | 5676 | Besiktas vs Kayserispor | 1.52 | 4.23 | 5.50 |
| 19:30 | 1085 | Crystal Palace vs Everton | 2.27 | 3.15 | 3.30 |
| 19:30 | 3868 | Eintracht Frankfurt vs Bayer Leverkusen | 3.18 | 3.67 | 2.09 |
| 20:00 | 2315 | Napoli vs Empoli | 1.35 | 5.41 | 7.41 |
| 20:00 | 2384 | Sassuolo vs Lazio | 2.67 | 3.47 | 2.52 |
| 20:00 | 3652 | Sparta Prague vs Bohemians | 1.29 | 5.78 | 9.17 |
| 20:00 | 3935 | Midtjylland vs Brondby | 1.89 | 3.51 | 3.51 |
| 20:30 | 2021 | Olympiakos vs Aris Salonica | 1.43 | 4.43 | 6.70 |
| 20:30 | 2030 | CFR Cluj vs CS Mioveni | 1.31 | 4.82 | 9.25 |
| 20:30 | 3790 | KAA Gent vs Racing Genk | 1.84 | 3.60 | 3.95 |
| 20:30 | 5244 | Betis vs Real Sociedad | 2.30 | 3.25 | 3.15 |
| 21:00 | 2836 | Famalicao vs Benfica | 6.90 | 4.53 | 1.41 |
| 22:00 | 5485 | NEC Nijmegen vs PSV Eindhoven | 7.25 | 5.09 | 1.34 |
| 22:45 | 4172 | Inter vs Cagliari | 1.19 | 7.22 | 12.03 |
| 22:45 | 4314 | Paris St Germain vs Monaco | 1.50 | 4.49 | 5.62 |
| 23:00 | 1573 | Real Madrid vs Atletico Madrid | 2.19 | 3.29 | 3.34 |
| 23:00 | 4558 | Brugge vs Zulte Waregem | 1.19 | 7.07 | 10.81 |
| 23:30 | 1750 | Porto vs Sporting Braga | 1.49 | 4.35 | 5.73 |
| 23:30 | 2762 | Atletico Mineiro vs Atletico Pr | 1.45 | 4.03 | 6.15 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo



Jumapili Desemba 12, 2021

Nipashe

**Rangnick: Sitamshawishi Pogba kubaki**

HABARI UK 21




Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' (kulia), akiwatoka wachezaji wa Simba katika mchezo wa ligi Kuu Tanzania baina ya timu hizo, uliopigwuliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BAHATI YAO

## ●●●Barbara azuiwa getini, Simba, Yanga zaupiga mwingi hadi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

Bahati yao!

PAMBANO la watani wa jadi nchini, Simba na Yanga, jana lilimalizika kwa suluhu ya bila kufungana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, mechi iliyotawaliwa na ufundi na mbinu zaidi.

Baada ya miaka mingi, mashabiki wa soka waliokuwepo uwanjani na waliokuwa wakiangalia kwenye televisheni walishuhudia mechi isiyokuwa na matumizi makubwa ya nguvu kama ilivyozoeleka, badala yake makocha Pablo Franco wa Simba na Nasreddine Nabi wa Yanga waliwekeza kwenye mbinu na ufundi zaidi.

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya nane ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo, imefanya Yanga kuendelea kuongoza ligi ikifikisha pointi 20, ikishinda mechi sita na sare mbili, Simba nayo ikiendelea kujikita kwenye nafasi ya pili kwa kufikisha pointi 18, ikishinda mechi tano na sare tatu.

Yanga kama kawaida yake kwenye miaka ya hivi karibuni inapocheza dhidi ya Simba, ilianza pambano hilo kwa kasi na kufanya kulitia msukosuko lango la wapinzani wake na dakika ya tano tu, ilikuwa imeshafika langoni kwa Jesus Moloko kumuacha Mohamed Hussein 'Tshabala' na kumimina krosi ya hatari iliyopanguliwa na kipa Aishi Manula.

Dakika mbili baadaye, Simba ilijibu shambulio hilo, baada ya Meddie Kagere kumpa pasi Bernard Morrison nje ya eneo la hatari, akauweka mpira kifuani, akageuka na kuachia fataki kali lililopaa juu kidogo ya lango la Yanga.

Hilo ndilo shambulizi la maana pekee ambalo Simba ililifanya dakika zote za 45 za mwanzo, ambapo ilionekana kukaa nyuma ya mpira wakiwaachia wapinzania wao wakimiliki, lakini anapoupata wanafanya mashambulizi ya kushtukiza ambayo mengi yalikuwa yakiishia kwenye miguu ya mabeki wa Yanga na kurejea tena nyuma kukaba.

Kama angekuwa makini, Khalid Aucho angeipatia timu yake bao dakika ya 23, baada ya kupiga kichwa akiwa huru, mkwaju wa faulo uliopigwa na Saido Ntibazonkiza, ukatoka sentimeta chache juu ya lango la Simba.

Faulo hiyo ilitokana na Joash Onyango kumchezea madhambi Fiston Mayele pembeni, mashariki kwa uwanja wa Mkapa.

Fiston alikosa bao la wazi, alipobaki yeye na Manula, akaubetua kwa mguu ukatoka nje ya lango. Ni mpira uliomjia kutokana na shuti la Feisal Salum kuwababatiza mabeki wa Simba na kujikuta akibaki yeye na kipa, lakini alionekana kukosa utulivu.

Kipindi cha pili Simba ilionekana kubadilika na kuanza kuliweka kwenye heka heka lango la Yanga, na ilianza kwenye sekunde ya 35 tu wakati krosi ya Shomari Kapombe ilimkuta Kagere aliyepigwa kichwa, lakini kipa Djigui Diarra akaudaka kwa ustadi.

Simba iliwatoa Morrison, Kagere, na Kibu Denis na kuwaingiza Yusuph Mhilu, John Bocco na Rally Bwalya, huku Yanga ikiwatoa Moloko na Mayele, nafasi zao zikachukuliwa na Farid Mussa na Heritier Makambo.

Hata hivyo, dakika ya 49, nusura Yanga ipate bao, baada ya kutokea kizaazaa kwenye lango la Simba, lakini mabeki walifanikiwa kuokoa, kabla ya Ntibazonkiza kuwatoka mabeki wa Simba na kuachia shuti lililogonga nguzo ya pembeni dakika ya 59 na kukumkuta Mayele akiwa ameotea.

Bocco alikosa bao la wazi dakika mbili kabla ya pambano kumalizika, baada ya kushindwa kumalizia vema mpira uliotemwa na Diarra kutokana na shuti kali la Sadio Kanoute.

**BARBARA AZUIWA GETINI**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez na familia yake walizuiliwa kuingia uwanjani, aliamua kuondoka uwanjani hapo.

"Barua zinazoandikwa sio zangu zinaandikwa na taasisi ya (Simba SC), lakini naona wao wameichukua ni kitu cha kijinga kabisa," alisema Barbara wakati anaondoka uwanjani.

Hata hivyo, haikujulikana mara moja sababu ya kuzuiwa kwa mtendaji huyo wa Simba.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042